# Nipashe

Alhamisi Oktoba 29, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580383

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba :+255716500500
Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


**NEC** yatoa kauli madai ya kuwapo kwa kura bandia

UKURASA 3



**VIONGOZI** watoa ya moyoni baada ya kushiriki uchaguzi

UKURASA 4

UCHAGUZI 2020

# Matokeo yaanza



Mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli akipiga kura.



Mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu akipiga kura.

UKURASA 12



Mgombea urais wa ADC, Queen Sendiga akipiga kura.



Mgombea urais wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Seif Sharif Hamad akipiga kura.



Mgombea urais wa CCM Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi akipiga kura.




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


## Purukushani zaibuka mawakala kuzuiwa

UKURASA 2

## Halima Mdee aingia matatani

UKURASA 3


MICHEZO SIMBA: MAJEMBE YAMEREJEA RASMI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akipiga kura yake ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, wabunge, wajumbe wa baraza la wawakilishi na madiwani, katika kituo cha kupigia kura cha Bungi, Wilaya ya Kati Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Watanzania wafanya yao

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA jana walifanya uamuzi kupitia sanduku la kura kwa kuchagua diwani, mbunge na rais katika vituo mbalimbali nchini.

Uamuzi huo ulifanywa katika vituo vya kupigia kura 80,155 na miongoni mwa Watanzania waliojiandikisha 29,188,347 ambao walishiriki kuchagua rais mmoja, wabunge 390 na madiwani 5,350.

Wakati hayo yakifanyika, hadi sasa CCM ina mtaji wa wabunge wateule 28 na madiwani 870 waliopita bila kupigwa.

Uamuzi ulifanywa ndani ya sanduku la kura licha ya kasoro kadhaa zilizokuwapo kama mawakala wa baadhi ya vyama kuzuiwa kuingia kwenye vituo, kukamatwa, kujeruhiwa, huku wagombea wakijeruhiwa na kukamatwa na polisi kwa madai mbalimbali.

Kwa uchaguzi huo ndiyo atapatikana rais ambaye kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ataongoza kwa miaka mitano kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Tangu kuanza kwa uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1995, mtiririko wa kura baina ya wapinzani na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na idadi za kura kwenye mabano ni Benjamin Mkapa kura 4,026,422 (asilimia 61.82) akifuatiwa na Augustino Mrema wa NCCR-Mageuzi kwa kura 1,808,616 sawa na asilimia 27.77.

Uchaguzi wa mwaka 2000, Mkapa alikuwa anawania kipindi chake cha pili alipata kura 5,863,201 ambazo ni asilimia 71.74, huku mpinzani wake wa karibu, Prof. Ibrahim Lipumba wa Chama cha Wananchi (CUF) akipata kura 1,329,077 sawa na asilimia 16.26.

Katika uchaguzi wa mwaka 2005 mgombea wa CCM alikuwa Jakaya Kikwete ambaye alishinda kwa kura 9,123,952 sawa na asilimia 80.28, huku mshindani wake wa karibu, Prof. Lipumba wa CUF akipata 1,327,125 sawa na asilimia 11.68.

Katika uchaguzi wa mwaka 2010 ikiwa ni kipindi cha pili, Kikwete alipata kura 5,276,827 sawa na asilimia 62.83, huku mpinzani wake wa karibu Dk. Willibrod Slaa kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akipata kura 2,271,491 (asilimia 27.05).

Mwaka 2015 Rais John Magufuli kwa tiketi ya CCM alipata kura 8,882,935 sawa na asilimia 58.46, huku mshindani wake, Edward Lowassa wa CHADEMA akipata kura 6,072,848 sawa na asilimia 39.97.

# Purukushani zaibuka mawakala kuzuiwa

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya mawakala wa vyama vya siasa kwenye vituo vya kupigia kura wamelalamikia kuzuiwa kuingia kwenye vituo hivyo na wengine watatu kukamatwa na askari polisi kwa madai ya kutokuwa na barua za utambulisho kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Waliokamatwa na Jeshi la Polisi ni mawakala watatu wa Chama cha Wananchi (CUF), ACT -Wazalendo, CHADEMA na Ofisa Mtendaji mmoja wa serikali katika Jiji la Tanga, baada ya kuingia katika vituo vya kupigia kura wakiwa hawana barua za utambulisho wa Tume.

Dosari hiyo ya kukosekana kwa barua za mawakala imejitokeza kwenye vituo mbalimbali vya kupigia kura Jimbo la Tanga Mjini.

Hatua hiyo ya sintofahamu imeleta kutoelewana baina ya mawakala na wasimamizi wa vituo.

Mawakala waliokutwa na sakata hilo ni kutoka vyama vya ACT-Wazalendo, Chama cha Wananchi (CUF), CHADEMA na NCCR-Mageuzi.

Kwa mujibu wa maelezo ya baadhi ya mawakala hao, walielezwa kuwa barua hizo watazipata kwenye ofisi za watendaji wa kata, lakini wamedai watendaji wanawazungusha na kudai hawana barua.

"Sisi tunashangaa iweje mawakala wa CCM wote wawe na barua, lakini sisi wa upinzani barua zetu zisijulikane zilipo...hii si haki kabisa Mkurugenzi mwenyewe wa Jiji ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo alisema tutazikuta huko sasa inakuwaje hali ni tofauti," alihoji Fadhili Bakari, mgombea udiwani Kata ya Mzingani kupitia ACT-Wazalendo.

Walisema kinachowashangaza ni zoezi la kupigia kura linaendelea huku wakiwa hawajui hatima yao.

Kufuatia sintofahamu hiyo, Jeshi la Polisi lililazimika kuwachukua baadhi ya mawakala, Mgeni Mayombo (ACT-Wazalendo), Idrissa Abubakar (CUF) na Omary Ally (NCCR).

Mawakala hao walikuwa katika ofisi ya Mtendaji Kata ya Ngamiani Kusini, kituo cha Muungano B namba 2518802 - kata mpya 2.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Blasius Chatanda, alisema mawakala wa vyama vya siasa na baadhi ya wafuasi wa vyama hivyo walikamatwa kutokana na kuibua sintomfahamu kwenye vituo vya kupigia kura, na kwamba wako katika mikono salama.

Alisema wanashikiliwa na jeshi hilo kwa ajili ya mahojiano, akifafanua kuwa uamuzi wa kuwakamata na kuwashikilia ulitokana na kuzuka tafrani katika baadhi ya vituo vya kupigia kura, huku baadhi ya wafuasi wa vyama hivyo wakijaribu kuzuia wananchi kupiga kura kwa kufunga milango.

Kamanda Chatanda alisema mawakala na wafuasi hao wa CUF, CHADEMA na ACT-Wazalendo walikamatwa katika vituo vya Tongoni na Ofisi ya Mtendaji ya Kata ya Ngamiani Kusini.

"Ni kweli wapo baadhi ya wafuasi wa vyama vya siasa, tunawashikilia kwa mahojiano kwa sababu kulikuwa na kutoelewana kwenye vituo walivyokuwapo. Sasa jambo hilo tuliona kwamba lingeweza kuleta vurugu kama tungewaacha waendelee kuwapo kwenye maeneo hayo," alisema.

Jijini Dar es Salaam, mmoja wa mawakala kutoka Chama cha ACT-Wazalendo, Khamis Sungura, alidai jina lake lilipangwa kituo cha kupigia Chuo Kikuu Huria, Jimbo la Kinondoni, lakini alizuiwa kuingia kituoni na msimamizi wa uchaguzi.

"Jina langu linaonyesha ni kituo hiki namba nne nimefika hapa mapema nimekataliwa kuingia hapa, hadi niwe na barua," alisema Sungura.

Akilalamikia hali hiyo mgombea ubunge Jimbo la Kinondoni, kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Saed Kubenea, alidai mawakala zaidi ya 200 kati ya 790 wa jimbo hilo, wamezuiwa kuingia vituoni kwa sababu hizo.

"Ni sababu ambazo hazina msingi, wanaambiwa waje na barua kitu ambacho ni kinyume kabisa na utaratibu, mpango ulipangwa. Imani na kura zetu humo ndani haupo hatuna wasimamizi wa chama chetu," alidai Kubenea na kuongeza...hili limejitokeza vituo vya Hananasifu na Mwenge."

Alidai kumtafuta msimamizi wa uchaguzi Kinondoni, lakini hakupata majibu.

### WAPIGAKURA WANENA

Kwa upande wao wapigakura wa vituo mbalimbali vilivyotembelewa na Nipashe, akiwamo mkazi wa Mkunguni A, Symfroza Elias, alisema uchaguzi huu umekuwa na vituo vingi tofauti miaka ya nyuma, ingawa tatizo lipo kwenye majina ya wapigakura kutoonekana vizuri.

"Nimefika saa 2:30 asubuhi, nimekuja na kijana wangu ili kuniangilizia jina. Isingekuwa yeye ningekata tamaa majina yanachanganya."

David Mwaisela, mkazi wa Mwananyama Kisiwani, alisema alifika kituoni mapema na kupiga kura bila kuchukua muda mrefu.

"Sasa tofauti na miaka mingine foleni zilikuwa ndefu, wazee leo (jana) tumepewa kipaumbele," alisema Mwaisela.

Vile vile, eneo la Tabata Shule, jijini Dar es Salaam, Nipashe ilishuhudia purukushani baada ya baadhi ya mawakala kuzuiwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura kwa kukosa barua.

Katika majimbo ya Kawe na Kinondoni, mawakala walishindwa kuingia kwenye vituo vyao na wengine kubadilishiwa vituo na kupangwa vya mbali walikolazimika kutembea umbali mrefu.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Kata ya Hananasifu, Petro Nyoni, alisema wakala wao wa kituo cha kupigia kura Mkunguni A wamebadilishiwa bila kupewa sababu.

Alisema wakala aliyepangwa na chama katika kituo hicho jina lake limeondolewa na kuwekwa jina la wakala mwingine bila muhusika kujua.

"Wakala Abdulbaswat Shwaibu, tumempanga kituo cha ofisa mtendaji A-3 baada ya kufika amezuiliwa na kuambiwa Issa Mbilinga ndiyo kapangwa, wakati sisi hatujampanga, wametubadilishia majina ya mawakala wetu bila kuwa na taarifa," alidai.

Alidai kuwa kitendo walichofanyiwa ni cha uonevu kwa kuwa walipeleka mwongozo wao wa majina ya mawakala, lakini kwenye vituo hakuna mawakala.

Nyoni alisema hata wakala ambaye amefika eneo la tukio la kupiga kura ameambiwa awasilishe barua ya kitambulisho, kitu alichodai kuwa hakipo kwenye kanuni.

Mohamed Kalembo, wakala wa CHADEMA aliyeteuliwa kwa ajili ya kusimamia kituo cha Ofisa Mtendaji Kawe, alidai walipoapishwa, alijaza fomu yenye kielelezo cha picha yake wakajulishwa fomu watazikuta kituoni.

"Cha ajabu fomu hazijafika hadi saa nne asubuhi, ukiwaangalia mawakala wa CCM wao wana fomu ila mimi nimezuiliwa," alidai.

Kalembo alidai baada ya muda, fomu ziliwasili bila majina yao jambo lililowashangaza.

Nipashe ilishuhudia baadhi ya maeneo wananchi wakijitokeza kupiga kura, huku kukiwa na ulinzi wa askari wa Jeshi la Polisi, Magereza na Mgambo wakiangalia usalama.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi walisema uchaguzi wa mwaka huu ni wa tofauti na miaka mingine kwa kuwa hakuna foleni, jambo linalowawezesha kufika kituoni kupiga kura na kuondoka kwa haraka.

Athumani Kitogo, mkazi wa Mwananyamala Kisiwani, alisema alifurahi kufika na kupiga kura ikilinganishwa na uchaguzi wa miaka iliyopita kuwa na foleni iliyowakatisha tamaa.

"Hali ya leo ya uchaguzi ni tofauti na miaka yote kwanza kuna utulivu na hakuna foleni nimefurahi nimefika sijatumia hata dakika 10 nimeshapiga kura yangu," alisema Kitogo.

Hata hivyo, alisema kuna tatizo kwa baadhi ya wasimamizi kutojua majukumu yao na kuleta shida kwa wapigakura.

"Nimefika nikauliza nikajibiwa natakiwa niende kituo kingine, wakati natakiwa kupiga kura hapa Shule ya Msingi Mchangani. Nilivyofuatilia kwa mwingine akanisaidia kunielekeza darasa la kwenda kupiga kura," alisema.

### VITUKO

Mmoja wa wapigakura, aliyejitambulisha kwa jina la Joseph Lyamuya, inadaiwa alifika kituo cha kupigia kura Makongo Juu, akiwa amelewa na kuwalazimu wasimamizi kumpa kipaumbele cha kupiga kura.

Musa Haji ambaye alikuwa amepanga foleni moja na Lyamuya, alisema aliamua kumpa taarifa askari polisi aliyekuwa jirani baada ya kuona anapata usumbufu.

"Huyu jamaa kaja kituoni kalewa, anahangaika hatulii katika foleni," alilalamika Haji.

Askari polisi aliyetoa msaada huo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, aliiambia Nipashe kuwa ameempa kipaumbele cha kupiga kura, ili kuondoa mzozo.

"Nimeona ili kuondoa hili, akae mbele akapige kura aondoke, ili kuweka hali shwari. Mtu kama huyu akiendelea kukaa kwenye foleni atakwaza wenzie," alisema askari huyo.

Akihojiwa na Nipashe sababu ya kuwa katika hali hiyo, Lyamuya alidai amevurugwa baada ya baadhi ya mawakala wa CHADEMA kuzuiwa kusimamia upigaji kura.

***Imeandikwa na Christina Mwakangale, Beatrice Shayo (Dar) na Lulu George (Tanga)***

# NEC yatoa kauli madai kura feki

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imekanusha kuwapo taarifa za kuwapo kwa kura bandia zilizoingizwa katika baadhi ya vituo vya kupigia kura.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wake, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa upigaji kura za Rais, wabunge na wadiwani katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema hayo baada ya kuwapo kwa madai ya kuwapo kwa kura bandia zilizoingizwa katika maeneo kadhaa nchini kwenye vituo vya kupigiwa kura. Madai hayo yalisababisha baadhi ya wagombea wa ubunge wa vyama vya upinzani kukabiliana na polisi baada ya kutokea ubishi.

"Tume inaomba Watanzania kuyapuuza madai hayo kwani hayana ukweli wowote. Tunafuatilia kila hatua ya upigaji kura na tuna taarifa kutoka sehemu mbalimbali," alisema Jaji Kaijage.

Awali, mgombea ubunge wa Kigoma Mjini kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alidai kuwa katika kituo kimoja, kulikuwa na mfuko ambao uliingizwa ukiwa na karatasi ambazo zimeshapigwa kura.

Mbali na Kigoma Mjini, madai kama hayo yaliibuka jijini Dar es Salaam katika Jimbo la Kawe kituo cha Kawe Mzimuni baada ya mgombea ubunge wa Chama cha Demokrasia Maendeleo (CHADEMA), Halima Mdee kudai kuwa kulikuwa na kura bandia zilizoingizwa.

Hatua hiyo ilisababisha purukushani na hatimaye upigaji kura kusimama kwa muda huku Mdee akipelekwa kituo cha polisi Kawe na kuhojiwa kisha kuachiwa.

Aidha, jijini Mwanza katika Jimbo la Nyamagana, ziliibuka tuhuma za mwananchi mmoja aliyadaiwa kupeleka mfuko uliojaa karatasi za kura akidai kuwa ni chakula kwa ajili ya mawakala wa CCM.

Nako mkoani Kagera, Mgombea Ubunge kwa tiketi ya CHADEMA katika jimbo la Bukoba Mjini, Chief Kalumuna, aliibua madai ya kukamatwa kwa masanduku mawili ya kura zilizopigwa katika maeneo ya Kahororo na Rugambwa.

Akizungumza na Nipashe mgombea huyo alisema kuwa alipata taarifa hizo kutoka kwa watu wake wa karibu wanaomsaidia kufuatilia mchakato wa uchaguzi katika maeneo mbalimbali kuwa masanduku hayo yamekamatwa na kuchukuliwa na polisi.

Hata hivyo, Msimamizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Bukoba Mjini, Limbe Moris, amekanusha taarifa hizo kuwa ni za uzushi.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alikanusha jeshi hilo kukamata masanduku hayo na kusisitiza kwamba hazina ukweli wowote.




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipiga kura kwa ajili ya kuchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, wabunge, wajumbe wa baraza la wawakilishi na madiwani katika kituo cha SOS Mombasa, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMR**

# Mbaroni akidaiwa kuficha kura kwenye chakula

**Na Richard Makore,** MWANZA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, mwanamke amekamatwa na kura zilizopigwa akitaka kuziingiza katika kituo cha kupigia kura cha Mbugani, Jimbo la Nyamagana mkoani Mwanza.

Nipashe ilishuhudia mwanamke huyo akiwa amewekwa chini ya ulinzi na Jeshi la Polisi, ambalo pia limethibitisha kuwapo kwa tukio hilo.

Baadhi ya wananchi waliokuwapo kituoni huko walisema jana kuwa mama huyo aliingia kituoni akiwa na kikapu ambacho juu yake alikuwa ameweka chakula, lakini chini kukawa na karatasi zilizopigwa kura tayari.

Akizungumza muda mfupi baada ya kukamatwa kwa mama huyo akiwa na karatasi hizo, Mgombea Ubunge wa jimbo hilo, John Pambalu (CHADEMA) alidai walikamata kura za namna hiyo katika kata nne jana.

Alisema katika maeneo hayo, walifanikiwa kuzuia kura zikizopigwa nje ya kituo kuingizwa kwenye masanduku halali ya kura.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alikiri kukamatwa kwa mama huyo akiwa na kura zilizopigwa na kusema kuwa wanaendelea na uchunguzi wa suala hilo.

**Katika maeneo hayo, walifanikiwa kuzuia kura zikizopigwa nje ya kituo kuingizwa kwenye masanduku halali ya kura.**

# Mdee akamatwa madai kuzusha vurugu

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA ubunge wa Kawe kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Halima Mdee, jana alikamatwa kwa tuhuma za kusababisha vurugu zilizosababisha upigaji kura kusimama kwa muda.

Wakati Mdee yakimkuta hayo, mkoani Tanga, familia ya mgombea ubunge kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF) Jimbo la Tanga Mjini, Mussa Mbaruku, inashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano baada ya kutokea vurumai kwenye kituo cha kupigia kura.

Mdee alikutwa na mkasa huo katika kituo cha kupigia kura cha Kawe Mzimuni baada ya kuwapo madai kwamba kulikuwa na kura bandia zilizoingizwa kituoni hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Edward Bukombe, amesema mgombea huyo alikamatwa na kuhojiwa katika Kituo cha Polisi cha Kawe kisha kuachiwa.

Pamoja na mkasa huo uliosababishwa kwa kiasi kikubwa na kupishana kwa kauli baina ya mdee na polisi, Kamanda Bukombe alisema Kinondoni hali iko shwari.

"Kinondoni iko shwari hakuna aliyepigwa zaidi ya kurushiana maneno maana Mdee alimshuku askari wakapishana maneno ndipo akachukuliwa kwa ajili ya kuhojiwa," alisema.

### MAMBOSASA ALONGA

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema tathmini ya uchaguzi kwa jiji hilo imeendelea kuwa shwari na hawajatumia bomu hata moja kipindi chote cha kampeni hadi upigaji kura.

Kuhusu madai ya karatasi za mpigakura kukamatwa Kawe, alisema bado hayajamfikia na kueleza kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeyafafanua kuwa ni habari za mtaani.

"Zikithibitika kama ni kweli tutafungua jalada na kupeleleza na kuangalia kitendo kilichofanyika kina ni cha jinai hatua za kisheria zitachukuliwa.

"Yapo matukio mawili mmoja amekamatwa Kimara akiwa na kisu na sare za mgambo ambazo siyo za kwake na upelelezi unaendelea, Mbagala yupo kijana alipiga picha kituoni siyo mwandishi wa habari, alikwenda kutengeneza vurugu, amekamatwa."

Kuhusu kukamatwa kwa Mdee, alisema alikamatwa na kuhojiwa kwa kitendo cha kwenda eneo la kupiga kura na kuzuia watu wasitekeleze hilo.

"Sababu zake tuliziona ni za kihuni zaidi, aliona mtu kavaa 'kabegi lake' akasema uchaguzi usiendelee, wapo watu wametoka mkoani kuja kupiga kura kwa sababu alijiandikishia hapa, akimaliza anarudi alikotokea, kupiga marufuku mtu asije na begi ni kitendo cha kihuni.

"Alikwenda mbele zaidi akajitwalia madaraka kuzuia watu wasipige kura, hicho ndicho kilifanya achukuliwe apewe elimu na kuonywa kwa sababu hayamjengei heshima kwa mgombea kwa kiti hicho cha ubunge."

### MGOMBEA, FAMILIA MATATANI

Kutoka Tanga, familia ya Mbarouk inashikiliwa na polisi kwa mahojiano baada ya kutokea sintofahamu kwenye kituo cha kupigia kura, Kata ya Ngamiani Kusini jijini humo.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe, Mbarouk ambaye alikuwa Mbunge wa Jimbo la Tanga kwa kipindi cha miaka mitano, aliwataja ndugu zake hao kuwa ni mama yake mzazi, Fatuma Hassan (70), dada zake Changa Bakari, Mwanaidi Bakari na Mwanakombo Bakari.

Familia hiyo ilikamatwa baada ya kuzuia kuingia kwenye chumba cha kupigia kura, ambapo walitaka kusimama kama mawakala wa mgombea huyo na ndipo walipodaiwa kukosa barua za utambulisho.

"Wao walikuwa ni mawakala wangu, lakini walizuiwa kwa sababu mtendaji hakuwapa barua na alipokuwa wakihoji ndipo Polisi walikuja kuwakamata," alisema Mbaruku.

Awali, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, alisema jeshi hilo linawashikilia mawakala watu kadhaa kutokana na vurugu zilizojitokea katika kituo cha kupigia kura kwa ajili ya mahojiano.

Kamanda Chatanga, licha ya kutowataja majina, alisema watu hao walikuwa baada ya kufikishwa kituo cha polisi, walihojiwa na baadaye kuachiwa.

***Imeandikwa na Christina Mwakangale, Romana Mallya, DAR na Lulu George, TANGA***

# JPM: Kuna maisha baada ya uchaguzi

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais, John Magufuli (CCM), amepiga kura na kuwataka wananchi kulinda amani iliyopo nchini, akikumbusha kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi.

Dk. Magufuli (pichani) jana alipiga kura katika Kituo cha Idara ya Maji kilichoko Chamwino mkoani Dodoma, akiwasili kituoni huko majira ya 3:59 asubuhi akiambatana na mkewe, Janeth Magufuli.

Baada ya kupiga kura, Dk. Magufuli alisema: "Ninawapongeza Watanzania kwa kuiona siku ya leo (jana) ya demokrasia. Ninawaomba tuendeleze kuitunza amani kwa sababu kuna maisha baada ya uchaguzi."



Mkoani Lindi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipiga kura kijijini kwake Nandagala wilayani Ruangwa. Majaliwa ambaye ni mbunge mteule wa Ruangwa, alipiga kura kwenye kituo cha Shule ya Msingi Nandagala alikofika akiwa na mkewe, Mary Majaliwa.

Baada ya kupiga kura, Waziri Mkuu alisema kupiga kura ni haki ya msingi na anamshukuru Mungu kwamba upigaji kura ulikuwa unafanyika salama.

"Ninamshukru Mungu nimeweza kushiriki haki yangu ya msingi ya kumchagua kiongozi ninayempenda ili aweze kuliongoza taifa hili.

"Kwa hapa Nandagala, mbunge na diwani walishapita bila kupingwa. Kwa hiyo leo (jana) nimepiga kura moja tu ya kumchagua Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Waziri Mkuu ambaye aliwasili kituoni saa 4:20 na kujipanga foleni yeye na mkewe, alifuata taratibu kama wananchi wengine na akapiga kura saa 4:53. Aliondoka kituoni huko saa 5:00 asubuhi.

Akizungumzia utaratibu mzima wa upigaji kura, Majaliwa alisema ulikwenda vizuri na akawapongeza wasimamizi wa kituo hicho kwa sababu alikuta kuna utulivu na watu walikaa kwenye foleni wakisubiri kuingia ndani.

"Nimekuta watu wanafuata utaratibu, wanapatiwa maelekezo, vitambulisho vinahakikiwa, ni jambo la kujivunia. Amani kwetu bado ni tunu ambayo hatutakiwi kuidondosha chini ikaharibika.

"Ninatoa wito kwa Watanzania tujitokeze tukapige kura ili tupate viongozi wa ngazi zote ambao watatuongoza. Ni nafasi muhimu, ukiikosa leo (jana), hutaipata tena kwa miaka mitano ijayo," alisema.



Wananchi wakisubiri kupata maelekezo ili kupiga kura katika kituo cha Ofisa Mtendaji Kata ya Kawe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maalim, Mwinyi wanena baada ya kura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAGOMBEA wa urais wa Zanzibar wanaoelezwa kuwa ndio wanaochuana, Dk. Hussein Ali Mwinyi (CCM) na Maalim Seif Sharif Hamad (ACT-Wazalendo) wamejitokeza kupiga kura na kuelezea matarajio yao.

Dk. Mwinyi na Maalim Seif walipiga kura katika vituo tofauti wakiwa wametofautiana nusu saa katika vituo vya uchaguzi.

Dk. Mwinyi alipiga kura saa 2:30 asubuhi katika kituo cha Kariakoo akitanguliwa na Maalim Seif Sharif Hamad aliyepiga kura majira ya 2:00 kituo cha Garagara, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Baada ya kumaliza kupiga kura, Maalim Seif, aliwaambia waandishi wa habari kuwa suala la kukubali matokeo litategemea na mazingira ya uchaguzi utakavyokwenda ikiwamo haki ya wapigakura kuzingatiwa pamoja na sheria za uchaguzi.

"Kupata haki ya kusimamia matokeo ya chama na mgombea na si kuwatoa kama ilivyojitokeza katika uchaguzi wa kura ya mapema juzi," alisema huku akishukuru pamoja na kuwapo mvua, wananchi wengi wamejitokeza mapema vituoni.

Dk. Mwinyi kwa upande wake, alisema katika ushindani kuna kushinda na kushindwa, lakini yeye yuko tayari kuyapokea matokeo kama yatakavyokuwa licha ya kwamba ana matumaini makubwa ya kushinda.

Hata hivyo alisema amesikitishwa na vitendo vya vurugu vilivyojitokeza juzi katika kura ya mapema na kuwataka wananchi kuendelea kudumisha amani wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.

"Jukumu la ulinzi na usalama ni la vyombo vya ulinzi, viongozi na wananchi, tudumishe amani yetu kwa maendeleo ya Zanzibar," alisema Dk. Mwinyi.

Alieleza kuwa anamatumaini ya kushinnda kwa sababu Chama Cha Mapinduzi kimefanya kampeni vizuri za kutangaza ilani yake pamoja na mwitikio wa wananchi wakati wa kampeni hizo.

Uchaguzi Mkuu umefanyika huku mvua zikinyesha na kukatika, lakini wananchi waliendelea kujitokeza kwa wingi huku idadi kubwa ya kinamama wakionekana katika vituo vya kupigia kura.

## Wafunga biashara kuwahi kupiga kura

**Na Julieth Mkireri,** PWANI

BAADHI ya wananchi katika Mji Mdogo wa Mailimoja, Jimbo la Kibaha Mjini, jana walifunga maduka kwa zaidi ya saa nne kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kuwahi kupiga kura.

Nipashe ilitembelea eneo la Maili Moja na kushuhudia maduka yakiwa yamefungwa hadi saa tano, huku kwenye vituo vya kura katika eneo la Maili Moja B vikiwa wazi.

Ally Huseein, mmoja wa wananchi wa eneo hilo, alisema baadhi ya wananchi walichelewa kufungua biashara zao, ili kushiriki upigaji kura.

Katika Mji wa Mlandizi, Jimbo la Kibaha Vijijini, hadi majira ya saa tano baadhi ya vituo havikuwa na watu, huku vingine vikiwa na idadi chache ya wapigakura.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa watu wengi waliwahi asubuhi na kupanga foleni kupiga kura mapema na kurejea nyumbani kwao na hakuna wananchi waliobaki kituoni kulinda kura.

Katika kituo cha Shule ya Msingi Mtongani Mlandizi, baadhi ya wananchi walijitokeza kupiga kura huku wakiwa hawana vitambulisho.

Asha Abdallah (71), alisema kitambulisho chake cha kupigia kura kimepotea, hivyo kuomba kupiga kura bila kuwa na kitambulisho jambo ambalo lilishindikana

Mratibu wa uchaguzi Mkoa wa Pwani, Gerald Mbosoli, alisema mkoa huo una vituo 2,960 na wapigakura 991, 880.

## Wasusa kupiga kura

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya vijana katika Manispaa ya Shinyanga, wamesusa kupiga kura wakidai nchi iwe na tume huru ya uchaguzi, ili wagombea wanaoshinda kwa haki wawe wanatangazwa.

Wakizungumza na Nipashe jana mjini hapa, vijana hao walidai kuwa licha ya kuwa na vitambulisho vya kupiga kura, wameona hakuna umuhimu wa kupiga kura kwa kuwa ni sawa na kupoteza muda kwa kuwa hakuna tume huru ya uchaguzi.

Shadrack Joseph, mkazi wa Ngokolo mjini hapa, alisema kwa tume iliyopo, washindi wa uchaguzi wanajulikana hata kabla ya kupigwa kwa kura.

Alisema kuwa bila kuwapo tume huru ya uchaguzi, kamwe uchaguzi hauwezi kuwa wa haki na ndiyo sababu iliyomfanya asuse kwenda kupiga kura jana.

"Utaona baadhi ya vijana hapa mjini tunaendelea na shughuli zetu za kutafuta riziki na hatujaenda kupiga kura. Hatupigi kura kwa sababu wagombea wanaoshinda kwa haki katika jimbo hili la Shinyanga hawatangazwi, matokeo yake tunachaguliwa wabunge," alidai.

Paul Kitinya, mkazi wa Ndala mjini hapa, alisema hakwenda kupiga kura jana, akidai kuwa wagombea wanaoshinda, hawana msaada wowote kwa jimbo hilo.

Kitinya pia alisema jambo lingine linalomkatisha tamaa kupiga kura ni kutokuwapo kwa kile alichokiita kutendwa haki kwa wagombea wa vyama vyote.

# Wananchi wafurahishwa kuongezwa vituo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANANCHI wa kata mbalimbali Manispaa ya Morogoro wameishukuru serikali kwa kuongeza idadi ya vituo vya kupigia kura na kuwarahisishia kupiga kura mapema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi hao akiwamo Mwajabu Juma (85), alisema jana baada ya kupiga kura kuwa anashukuru kuwapo vituo viwili kwenye kituo chao cha Zahanati. Juma alisema anaamini uchaguzi wa mwaka huu ni mwepesi kutokana na hali ya utulivu aliyoiona jana, tofauti na wiki mbili zilizopita za kampeni.

"Michakato ya kampeni ilitupa wakati mgumu wa kuwa na hofu hata ya kupiga kura, lakini hali ni tofauti ukienda kupiga kura unapata nafasi upesi na kurudi nyumbani," alisema Juma.

Akizungumzia hali hiyo msimamizi wa uchaguzi Jimbo la Morogoro Mjini, Sheila Lukuba, alisema wamelazimika kuongeza vituo hadi kufikia 758, wakati mwaka 2015 kulikuwa na vituo 296.

Msimamizi Mkuu wa Kituo cha Zahanati Mbili, Dominica Simwanza, alikiri kutokuwa na foleni kwenye kituo hicho na kudai kuwa hali hiyo inatokana na nyongeza ya vituo kwenye maeneo mengi.

Alisema uchaguzi unaendelea vizuri kwa amani na watu wameonyesha mwitikio hadi saa sita watu 100 walikuwa wameshapiga kura.

Naye msimamizi mkuu wa kituo cha Azimio 3, Sophia Kilama, alisema wamekumbwa na tatizo moja la mpigakura kutoka Dar es Salaam kutaka kupiga kura ya rais jambo mbalo halikuwezekana baada ya kukosa mwongozo na mpigakura huyo alikubali kuondoka.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, hali ya mkoa ni shwari, uchaguzi unaendelea vizuri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema uchaguzi unaendelea vizuri hakuna vurugu zozote.

# Lissu: Siridhishwi uchaguzi, Lipumba adai kura siyo ya siri

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema haridhishwi jinsi Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilivyosimamia uchaguzi mkuu uliofanyika jana

Katika ukurasa wake wa Tweeter, Tundu Lissu aliyepigia kura katika Kituo cha Ntewa A, Shule ya Msingi Ntewa, Kata ya Ntuntu, jimbo la Singida Mashariki, wilayani Ikungi, mkoani Singida, aliandika:

"Siridhishwi namna Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilivyosimamia uchaguzi mkuu wa leo, kuna ukiukwaji mkubwa wa taratibu za uchaguzi."

**LIPUMBA AFUNGUKA**

Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, amesema kuwa kura iliyopigwa na Watanzania kwa sasa siyo ya siri kwa kuwa namba zimeandikwa kwenda kila karatasi ya mpigakura.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupiga kura katika kituo cha Kunduchi jijini Dar es Salaam, alisema kwa upigaji kura huo, hakuna usiri licha ya kutamkwa kuwa ni kura ya siri.

Profesa Lipumba alisema ameshangazwa na utaratibu wa kunakili namba ya mpigakura kwenye karatasi ya kupigia kura na kitini kinachobaki Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Siyo kura ya siri kwa sababu ile namba ya mpigakura inaandikwa kwenye karatasi ya kupigia kura, mtu akisoma namba na ukienda kwenye tovuti ya NEC unajua mpiga kura ni nani. Kwa hiyo kila kura inayopigwa itajulikana nani kampigia kani," alibainisha.

"Tuwe wavumilivu tujenge amani

Nimepata taarifa kuwa mawakala wengi katika vituo vya kupigia kura wamezuiwa, hii hali si nzuri," alisisitiza Prof. Lipumba.

Aidha, aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kutenda haki, huku akieleza kusikitishwa na mawakala wa vyama vya upinzani kunyimwa kuingia kenye vituo vya kupiga kura kushuhudia kinachoendelea, jambo ambalo alisema linatia doa uchaguzi.




Mkazi wa Kawe jijini Dar es Salaam, Aisha Mohamed, akitoka kupiga kura katika kituo cha Kawe Sokoni, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mamia ya wapigakura wakosa majina vituoni

**Na Wandishi Wetu**

MGOMBEA ubunge wa Mbeya Mjini, Tulia Ackson (CCM), amesema moja ya kero walizokutana nazo wapigakura jana, ni kutoona majina yao vituoni.

"Kuna baadhi ya maeneo mpigakura anaambiwa jina halipo, nimekutana na mtu mmoja amekwenda sehemu tano bila kuona jina lake, tumewatafuta wahusika walitafute hilo jina ili mwananchi huyu atimize haki yake," alisema Dk. Tulia alipozungumzia uchaguzi huo jana.

Alisema alipita vituoni kuhakikisha mawakala wa CCM na vyama vingine kama wamefika na kukuta mchakato unakwenda vizuri.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akizungumza baada ya kupiga kura, alisema ulinzi na usalama umeimarishwa.

Mgombea urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (CCM), alisema anaamini wananchi walisikiliza ilani ya CCM na walikipigia kura chama hicho ili kitekeleze kiliyoahidi kwao. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema amani na utulivu imeimarika na watu wengi walijitokeza kupiga kura jana.

"Viongozi watakaopita, nina jambo moja ninataka kuwaambia, kiongozi kazi yake ni kuongoza watu, siyo kujikweza na kudharau wananchi waliokupa nafasi kwa kukupigia kura.

Mgombea urais wa Chama cha Demokrasia Makini, Cecilia Mmanga, alipiga kura Mbagala jijini Dar es Salaam na kuwataka wananchi waendelee kudumisha amani na wasisikilize wanaowataka waingie barabarani.

Jijini Dar es Salaam, asubuhi kulikuwa na idadi kubwa ya wapigakura kwenye baadhi ya vituo vya kupigia kura Jimbo la Segerea, lakini mchana walipungua kwa kiwango kikubwa.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza kupiga kura katika jimbo la hilo, waliipongeza NEC kwa maandalizi mazuri na kuwapo kwa vifaa vya kutosha kulikowezesha wananchi kupata fursa ya kupiga kura bila tatizo.

Amina Rashid Mkazi wa Tabata Segerea, alisema vituo vilikuwa vya kutosha na watu walijitokeza kupiga kura bila vurugu.

Katika kituo cha Shule ya Msingi Mongo la Ndege iliyoko Jimbo la Ukonga, ilipofika saa 10:00 jioni, kituo kilifungwa na baadhi ya wapigakura waliochelewa walirudishwa.

Nipashe pia ilishuhudia baadhi ya maduka yakiwa yamefungwa.

Wakati hali ikiwa hivyo Dar es Salaam, mkoani Morogoro, Mgombea Ubunge Morogoro Mjini, Devotha Minja (CHADEMA), alisema hawana imani na uchaguzi huo kufuatia mawakala wao zaidi ya 100 kuondolewa kwenye vituo vya uchaguzi kwa makosa aliyodai yasiyoeleweka na baadaye kurudishwa.

Alisema wasimamizi wakuu wa vituo vya uchaguzi walitumia nafasi zao kuwaondoa mawakala hao kwa madai kuwa wamekwenda na kopi ya daftari la kudumu la wapiga kura, ambayo ni haki yao.

***Imeandikwa na Romana Mallya, Mary Geofrey (DAR) na Christina Haule (MOROGORO)***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wenye dhamana watende haki utangazaji matokeo

**JANA** Watanzania walipiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, huku ikikadiriwa kuwa wapigakura milioni 29 walikuwa na sifa ya kushiriki uchaguzi huo.

Kwa kiwango kikubwa, hali ya utulivu na amani ilionekana katika maeneo mengi ya nchi, ingawa kuna kasoro kadhaa zilizojitokeza na kulalamikiwa na baadhi ya vyama vya siasa.

Miongoni mwa kasoro hizo ni mawakala kukamatwa na Jeshi la Polisi katika baadhi ya maeneo kwa madai ya kuingia katika vituo vya kupigia kura bila kuwa na barua za utambulisho kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Vilevile, baadhi ya mawakala wa vyama walizuiwa kuingia katika vituo kwa madai hayo hayo, hali ambayo pia ilisababisha vyama husika kukosa mawakala katika vituo.

Aidha, baadhi ya vituo vilihamishwa bila Tume kutoa taarifa mapema, hali iliyosababisha usumbufu mkubwa kwa wapigakura, hivyo baadhi yao kuamua kuondoka kuelekea kwenye majukumu bila kupiga kura. Pia kuna matukio ya madai ya baadhi ya watu kujaribu kuingia vituoni wakiwa na kura ambazo zilishapigwa, lakini walidhibitiwa.

Suala la viapo vya mawakala lilizua mvutano takribani wiki moja iliyopita kati ya NEC na vyama kadhaa vya siasa, ingawa Tume iliahidi kuwa barua za mawakala zimgetolewa juzi katika ofisi za kata, ambako inadaiwa kuwa walizungushwa.

Hali hii inaacha maswali mengi kuliko majibu; kubwa ni kwa nini NEC haikulishughulikia suala hilo ili kuondoa malalamiko na mivutano isiyo ya lazima kabla ya siku ya uchaguzi jana?

Kadhalika, uamuzi wa kuhamisha vituo vya kupigia kura bila kutolewa taarifa kwa umma, ni jambo lingine ambalo kwa hakika limewakosesha haki ya msingi baadhi ya wapigakura, ambao walitumia muda wao kwenda katika vituo walivyojiandikisha kasha kuhakiki majina yao kabla ya jana.

Ni kweli kabisa kwamba pengine zilikuwapo sababu za msingi za kuhamisha vituo, isipokuwa uamuzi huo ulitakiwa kutolewa taarifa kwa umma, ili kuepusha usumbufu na malalamiko ya wadau wa uchaguzi. Sisi tunaamini kwamba katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia ya mawasiliano, malaka husika ingetoa taarifa na ili kila mmoja akafahamu kuhusiana na mabadiliko hayo.

Hata hivyo, tunawapongeza Watanzania waliojitokeza kuwachagua viongozi wanaowataka kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, wakiamini kwamba watawaletea maendeleo pamoja na kuwasilisha kero zao kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Pia wanastahili pongezi kutokana na kuonyesha utulifu licha ya kujitokeza kwa kasoro tulizozieleza, kinyume cha taarifa za uvumi zilizokuwa zinadai kuwa kuna vikundi vya vijana ambavyo viliandaliwa na baadhi ya vyama kuvuruga uchaguzi huo.

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa upigaji kura jana, kuanzia leo tunatarajia kuwa NEC itaanza kutekeleza wajibu wake wa kutangaza matokeo ya ubunge na udiwani kwa kata na majimbo yote.


Kimsingi, uchaguzi una ni mchakato kwa sababu una hatua kuanzia uteuzi wa wagombea ndani ya vyama, uteuzi wa NEC, kampeni, upigaji kura na kutangazwa kwa matokeo. Hata hivyo, utangazaji wa matokeo huwa na mvuto zaidi pengine kutokana na shauku ya wapigakura na umma kwa ujumla kutaka kujua wagombea waliopata dhamana ya wapigakura kuwaongoza.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kwamba kuanzia leo macho na masikio ya Watanzania wengi yataelekezwa kwa wakurugenzi wa halmashauri zote nchini ambao ndio wasimamizi wa uchaguzi kwa niaba ya NEC, ili kuwafahamu waliochaguliwa jana.

Tunaishauri NEC isimamie utangazaji wa matokeo unatawaliwa na haki; kikubwa washindi watangazwe mapema iwezekanavyo ili kuondoa hali ya hisia kwamba kuna njama za kuhujumu washindi, hivyo kutishia amani na utulivu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Acha mlo uliozoea, hamia namna hii

**MTINDO** wa baadhi ya watu wa kupenda kula chapati kwa maini na kisha kushushia ama soda au chai ya rangi, unaweza kuwa ni hatari kiafya, iwapo utaendelea kuendekezwa.

Kwanini hayo tena? Mtaalamu wa masuala ya lishe kutoka Jukwaa la Lishe Tanzania (PANITA), Jane Msagati, anaweka wazi zaidi kwa staili ya ushauri, ili wale waliouzoea, kuachana na ulaji wa aina hiyo.

Badala yake, anataka washushie juisi ya matunda, ili kusaidia mwili kuzalisha damu ya kutosha, kwa kuwa wanapokula hivyo, ni njia mojawapo ya kuiwekea uzito miili na kuwa na uwezo wa kufyonza virutubishi.

Mtaalamu huyo ametoa ushauri huo wiki iliyopita, alipozungumza kwenye kipindi cha Supa-Breakfast cha East Africa Radio na anawataka watu waepuke kula kwa mtindo huo, muhimu kwao kuangukia maelekezo ya wataalamu wa lishe.

Mlo kama soda na chai, mara nyingi hunazuia ufyonzaji wa virutubishi mwilini, hali inayosababisha miili kuwa na upungufu wa hivyo virutubishi. Ni vyema mtu anapokula chapati kwa maini, ashushie na juisi.

Juisi anayoisema ni ile iliyotengenezwa kwa matunda na maji yaliyo salama, kwa kuwa matunda ni vyanzo vizuri vya vitamin C, na msaada kwa mwili kuzalisha damu ya kutosha.

Nimekuwa mhamasishaji wa somo hilo kwa kirefu hayo yanayosemwa, lengo kuu ni kutaka kuhamasisha elimu zaidi kwa Watanzania, ili watambue umuhimu wa lishe bora na siyo ilmradi kula na kujaza, tumbo bila kujali suala la afya bora.

Elimu ya lishe bora na huduma nyingine za msingi kwa ajili ya afya ni haki ya kila mtu, ili aweze kutambua ni kipi cha kufanya ama kuacha, katika kuboresha afya yake.

Kwa mfano, ulaji wa chapati, chai na kushushia kwa soda, ni wa kawaida kwa Watanzania. Pia, nadhani wengi hawajui madhara yake na sasa inaelezwa kuwa ni muhimu kushushia kwa juisi.

Elimu kama hiyo inatakiwa kutolewa kwa wingi, ili kila mmoja wetu aipate, wale watakaoelewa na kuzingatia, iwasaidie kwa kuachana na ulaji wa mazoea, ambao umekuwa ni wa kawaida kwa watu wengi.

Kwanza, kuna umuhimu wa chakula kwa binadamu, hasa lishe bora ni muhimu zaidi, pia ieleweke kuwa chakula tafsiri yake ni kitu chochote kinacholiwa na kuupatia mwili virutubishi.

Vilevile lishe ni sayansi ya jinsi mwili unavyokitumia chakula na inahusisha jinsi mwili unavyosaga na unavyoyeyusha chakula na hatimaye virutubishi kufyonzwa na kutumika mwilini.

Hata Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alishawahi kuzungumzia suala la lishe duni aliposema inajumuisha ulaji usiofaa na mitindo ya maisha, ambavyo vinachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza, wote vijana na watu wazima.

Ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa, mtindo wake uko katika mabadiliko ya mitindo ya maisha na ulaji usiofaa, kama vile uzito uliozidi, viriba tumbo, shinikizo la damu na kisukari.

Anakiri serikali inatambua kuwa lishe bora ni msingi wa maendeleo ya taifa, hivyo ongezeko la magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza, linapaswa kudhibitiwa kwa kuzingatia ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha.

Mtendaji Mkuu huyo wa serikali, anaweka wazi kuwa watu watambue jitihada za serikali kwa kushirikiana na wadau kupambana na matatizo ya lishe, kwa kuwa nchi inakabiliwa na aina mbili za utapiamlo, ambazo ni lishe duni na iliyozidi.

Walengwa wakubwa wa lishe duni ni watoto chini ya miaka mitano, wanawake walio katika umri wa kuzaa hususani wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na vijana wenye umri wa kuvunja ungo.

Hiyo ni kwa sababu mahitaji ya virutubishi kwa ajili ya miili yao ni makubwa, ukilinganisha na ule unaohitajika na makundi mengine, hivyo ni vyema Watanzania kuzingatia umuhimu wa lishe bora.

Msisitizo mkubwa unapaswa kuwa katika elimu, ambayo ni msingi mkubwa kwa kila mmoja kutambua kile anachotakiwa kufanya na kile asichopaswa kufanya, katika eneo la lishe bora.

Hapo ndipo Watanzania wanapaswa kujua kwa kina faida za chakula kwa binadamu, ikiwamo kumtengenezea chembehai na kuzirudishia zilizokufa au kuharibika.

Vilevile kuna ukuaji akili za mwili, kuupa mwili nguvu, joto na uwezo wa kufanya kazi na kinga dhidi ya maradhi mbalimbali, hivyo inafanya suala la lishe bora kuwa na umuhimu wa kipekee na la kuzingatia.

Hilo litawezekana kwa kutolewa elimu ya kutosha kila kona ya nchi, ili kila mmoja atambue kuwa ulaji bora unaozingatia chakula mchanganyiko na kinachotosha mahitaji ya mlaji.

# Mbaroni madai kuingia na visu kituo cha kura

**Na Beatrice Moses**

MWANAMUME aliyetambulika kwa jina moja la Omary, amekamatwa na polisi baada ya kufika kwenye kituo cha kupigia kura akiwa amevalia gwanda nyeusi, na alipopekuliwa alikutwa na visu.

Nipashe ilishuhudia maofisa polisi wanne wa kituo cha uchaguzi Saranga Tanzanite wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam, ambapo alichukuliwa na kumwingizwa kwenye mojawamo ya vyumba kituoni hapo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na usalama Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, alithibitisha kukamatwa kwa mtu huyo.

"Ametambulika kwa jina moja, tayari gari la polisi limefika kumchukua kwa hatua zaidi, tunashukuru ulinzi na usalama wapo makini, wananchi wanaendelea vizuri na uchaguzi," alisema Muro.

Wakati huo huo wakala aliyetajwa kwa jina la Magreth Jacob wa CHADEMA, alitolewa nje ya kituo akidaiwa kuwa na simu wakati wamezuiwa kuingia nazo kwenye chumba cha kupigia kura.

Mwenyekiti wa CHADEMA Saranga, Athuman Sosoge, alilalamikia hatua hiyo, akidai kuwa msimamizi angemnyang'anya simu hiyo na kuhifadhi kisha angemwacha aendelee kufuatilia upigaji kura.

Pia kulizuka vikwazo kwa baadhi ya vituo kuchelewa kufunguliwa kutokana na vifaa kuchelewa kufika kwa wakati.

Omary Msangi, mkazi wa Mabibo, alisema alifika kwenye kituo cha NIT saa 11 alfajiri, lakini vifaa vilifuliwa saa 5 ndipo wakaruhusiwa kupigia kura.

"Nimepiga kura, nimefurahia utaratibu uliowekwa wa kupangwa kwa herufi ni mzuri, umepunguza msongamano vituoni," alisema Msangi.

Msimamizi wa kituo hicho, Henry Samuel, alisema kikwazo hicho kilipatiwa ufumbuzi, na wananchi walielewa na kuvumilia hatimaye kupigia kura kwa utulivu na amani.

Msimamizi Mkuu wa uchaguzi katika Jimbo la Kibamba na Ubungo, Beatrice Dominic aipohojiwa kuhusu hali ya upigaji kura katika eneo hilo alisema maeneo mengi umefanyika kwa utulivu.

"Naendelea kukusanya taarifa kutoka huko kwenye vituo, nami nipo natembelea kujiridhisha na hali ilivyo, baada ya hapo nitatoa taarifa," alisema Dominic ambaye pia ni Mkurugenzi wa Manspaa ya ya Ubungo.

**Ametambulika kwa jina moja, tayari gari la polisi limefika kumchukua kwa hatua zaidi, tunashukuru ulinzi na usalama wapo makini, wananchi wanaendelea vizuri na uchaguzi.**



Waziri Mkuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Kassim Majaliwa (wa pili kulia) na mkewe Mary (mbele yake), wakiwa kwenye foleni ya kusubiri zamu yao ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura cha Shule ya Msingi Nandagala, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**

# Vijana waonyesha mwamko kupiga kura

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

MWAMKO wa vijana kujitokeza kupiga kura katika Jimbo la Dodoma Mjini umeonekana kuwa mkubwa, huku dosari ndogo zikijitokeza ikiwamo kutoonekana majina ya baadhi ya wapigakura.

Dosari hizo zimejitokeza kwenye vituo vya Viwanda Sekondari, NHC, LAPF, Ipagala B, Shule ya Msingi Chang'ombe kwa wapigakura kudai kutoona majina yao licha ya kuwa na vitambulisho vya kupigia kura.

Tatizo lingine ni wapigakura kutohakiki majina yao mapema na kusababisha wengi wao kutumia muda mrefu kupata vituo vyenye majina yao.

Akizungumza na Nipashe, Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Msekeni Mkufya, alikiri kuwapo na dosari hiyo na kwamba zinaendelea kutatuliwa kadiri zinavyojitokeza kwa kuangalia kwenye mfumo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alisema kama mpigakura asipoona jina lake, wasimamizi wa uchaguzi wanafuatilia kwenye mfumo na kubaini majina yao yapo na kuwaruhusu kupiga kura.

"Sisi Dodoma tuna bahati, Tume ipo karibu, hivyo tukipata tatizo tunawasiliana nao na kutatua, kwa ujumla hali ni shwari, hii ya kutoona jina ni watu kuwa na wasiwasi wanaangalia haraka haraka," alisema.

Katika kituo cha NHC, mpigakura Pendo Mangala, alisema amezunguka sehemu zaidi ya mbili kutafuta jina lake.

Alisema, kituo alichojiandikishia jina mwaka 2015, katika daftari la kudumu kilihamishwa hivyo majina yaligawanywa kwenda kituo cha Viwandani Sekondari, LAPF na NHC Maghorofa Machafu.

"Nimekwenda Viwandani nimetafuta majina yangu sijayapata nimeambiwa nije huku Maghorofa Machafu, lakini kama tungepata taarifa mapema kutoka Tume basi tungeshahakiki ni kituo gani majina yetu yapo na leo tusingetumia muda mwingi kuyatafuta," alisema.

Katika hatua nyingine, mgombea ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Antony Mavunde, alipiga kura katika kituo cha Shule ya Msingi Chadulu na kuishukuru NEC kwa kuweka vituo vingi vya kupigia kura hali iliyoondoa msongamano.

Kuhusu kupokea matokeo, Mavunde alisema wananchi ndio wenye mamlaka ya nani awatumikie.

Katika kituo cha Kilimani, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema anafurahi kuona kundi kubwa la Watanzania wenye nia ya dhati kwa taifa lao kujitokeza katika vituo vya kupigia kura hali inayoonyesha walivyohamasika na uzalendo wa kupata kiongozi sahihi.

Alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuonyesha usalama kwa raia katika vituo vya kupigia kura.

Chifu Mkuu Kanda ya Kati, Henery Mazengo, aliipongeza NEC kwa kuandaa mazingira rafiki kwa wazee na watu wenye ulemavu.

Alisema vituo vya Kata ya Kikuyu Kusini, vimeweka mazingira mazuri kwa makundi yote maalum yanayopaswa kupewa kipaumbele.

Naye Maiko Salali, Mwenyekiti wa watu wenye ulemavu katika Taasisi ya Foundation for Disabilities, alisema mpaka sasa katika vituo vyote alivyotembelea hali ni nzuri, watu wenye ulemavu wamepewa kipaumbele.

Mkazi wa Chang'ombe B, Tatu Msambai, alisema utaratibu wa mwaka huu umekuwa bora zaidi na wa amani kuliko uchaguzi uliopita.

"Kwakweli nimefurahishwa zaidi na utaratibu wa mwaka huu kwani Tume imeweka utaratibu mzuri katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika, na kwa upande wa usalama uko vizuri, lakini hata mpangilio wa sehemu ya kupigia kura ni mzuri ambao ulitusaidia katika kuelewa vizuri na kufanikisha kupiga kura kwa weledi kabisa,'" alisema.

Christopher Mwita, mpigakura wa kituo cha Mtaa wa Chamwino, alisema amefurahishwa kuona vijana wenzake wamejitokeza kwa wingi kupiga kura.

Alisema idadi ya watu hasa vijana waliojitokeza kupiga kura ni kubwa kutokana na kuwapo kwa utaratibu mzuri wa kupiga kura.

Msimamizi wa uchaguzi kituo cha Wera Sekondari, Eniada Chigome, alisema tatizo lililojitokeza ni majina ya wapiga kura kutofautiana na kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Chigome, alisema tatizo hilo wamefanikiwa kulitatua kwa kuwapatia watu fomu namba 17, kwa ajili ya kuijaza ili waendelee na upigaji kura.

"Kwa kweli zoezi limekwenda vizuri kwa wakazi wa eneo hili, isipokuwa tatizo hilo ambalo nalo walifanikiwa kulitatua na waliokutwa na tatizo hilo kufanikiwa kupiga kura,"alisema Chigome.

Alisema dosari nyingine ni watu kutokuta majina yao kwenye vituo walivyojiandikisha na kuanza kutembea kituo kimoja hadi kingine kwenye kata husika kuyatafuta, wengine wanakata tamaa na hivyo kuamua kuwahi kwenye majukumu yao.

Aidha, watu wanapokuja na vitambulisho, lakini amejiandikisha kupiga kura katika mkoa mwingine.

Alisema watu hao wamekuwa wakiwaelewesha kwa wale wenye uwezo wa kuwahi maeneo waliojiandikisha walishauri waende wakipige kura katika maeneo hayo.

Hata hivyo, alisema zoezi hilo limekuwa rahisi kwao kutokana na wengi wa waliojitokeza mapema kupiga kura na kurejea nyumbani.

Msimamizi Mkuu Kituo cha Chang'ombe, Evalina Mario, alisema mwitikio katika kituo hicho ni mdogo, lakini pia ukosefu wa majina kwenye daftari imekuwa ni tatizo ambalo wasimamizi wamejitahidi kulitatua ili watu wapige kura.

Katika vituo ambavyo Nipashe ilitembelea ulinzi ulikuwa umeimarishwa na wananchi kupiga kura kwa utulivu na kuondoka.

***Imeandikwa na Augusta Njoji, Paul Mabeja na Renatha Msungu***

# MATUKIO YA UPIGAJI KURA

UCHAGUZI MKUU 2020



Mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli na mkewe Mama Janeth Magufuli wakiwa wamepanga foleni kwa ajili ya kupiga kura kwenye kituo cha Idara ya Maji, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, akipiga kura katika kituo cha Kinondoni Biafra, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Mgombea ubunge Jimbo la Kinondoni kupitia ACT-Wazalendo, Said Kubenea (katikati), akitoa malalamiko yake kwa waandishi wa habari, baada ya mawakala wa chama hicho, kuzuiliwa kuingia katika kituo cha kupiga kura cha Chuo Kikuu Huria, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wananchi wa Zanzibar wakiwa wamekusanyika wakisubiri kupiga kura katika kituo cha Garagara, Mjini Unguja jana. **PICHA: ANTHONY SIAME**



Baadhi ya mawakala wa Chama cha ACT-Wazalendo, wakiwa nje baada ya kuzuiliwa kuingia kituo cha kupiga kura cha Chuo Kikuu Huria, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MATUKIO YA UPIGAJI KURA



Baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo ya Masasi Mjini, Lulindi na Ndanda, wakiwa katika zoezi la uchukuaji wa vifaa vya uchaguzi kwenye ofisi za wasimamizi wa majimbo hayo, mjini Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASRI**



Mgombea ubunge wa Jimbo la Tanga (CCM), Ummy Mwalimu (kushoto), akihakiki jina lake kwenye kituo cha kupigia kura cha Shule ya Msingi Sahare, jimboni humo jana. **PICHA: OSCAR KASIMIRI**



Wananchi wakiwa wamekaa foleni wakisubiri kupiga kura katika kituo cha Hananasif Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mke wa mgombea urais kupitia CCM, Mama Janeth Magufuli, akipiga kura kwenye kituo cha Idara ya Maji, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mgombea ubunge Jimbo la Kinondoni, kupitia CCM, Abasi Tarimba, akipiga kura katika kituo cha Kinondoni Hananasif, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Waziri Mkuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Kassim Majaliwa, akipiga kura katika kituo cha kupigia kura cha Shule ya Msingi ya Nandagala wilayani Ruangwa, mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**

# Maelfu wajasiriamali wapata vitambulisho

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKOA wa Ruvuma umefanikiwa kutoa vitambulisho kwa wajasirimali wadogo 59,279 mwaka 2019 na vitambulisho 13,827 vimetolewa kwa wajasiriamali wadogo hadi kufikia Oktoba 23, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, wakati anafungua mkutano wa Baraza Maalum la Biashara la Mkoa wa Ruvuma mjini Songea.

Alisema mkoa umejikita kuhakikisha malengo ya serikali ya kuwa na uchumi wa viwanda yanafanikiwa na kwamba hadi kufikia Juni 2020, Mkoa wa Ruvuma ulikuwa na viwanda 3,485. Kwa mujibu wa Mndeme, kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa sita, viwanda vya kati 25, viwanda vidogo 190 na viwanda vidogo sana 3,264, na kwamba utekelezaji huo unaendelea kufanywa na sekta binafsi na sekta ya umma.

**Ili kukuza sekta ya viwanda, Mkoa wa Ruvuma umeendelea kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo, ambapo Julai 25, 2020 Mkoa uliandaa maonyesho ya viwanda na uwekezaji kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo.**

"Ili kukuza sekta ya viwanda, Mkoa wa Ruvuma umeendelea kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo, ambapo Julai 25, 2020 Mkoa uliandaa maonyesho ya viwanda na uwekezaji kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo," alisema Mndeme.

Alisema katika kongamano hilo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alizindua Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa, na kwamba mwongozo huo umesambazwa kwenye taasisi mbalimbali, ambapo hadi sasa wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza ni 22.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Emanuel Alphance, alilitaja lengo la kufanyika Baraza hilo la Biashara ni kufanya tathmini ya mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, na kuangalia mikakati na vipaumbele kwa upande wa sekta binafsi na umma katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alisema mfumo huo wa majadiliano kupitia mabaraza ya Taifa, mikoa na wilaya, unatokana na serikali kuwezesha sekta zote kushiriki katika mipango ya serikali sambamba na uwepo wa mazingira bora ya kufanya biashara.

Kwa upande wake, Yohana Nchimbi, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Ruvuma, alisema TCCIA kama sekta binafsi imenufaika kuanzia wafanyabiashara wa ngazi ya chini hadi juu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ya serikali ya awamu ya tano.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara wa Masoko Songea (UWABIMASO), alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuwawezesha wajasiriamali wadogo vitambulisho, ambavyo vimeondoa usumbufu mkubwa waliokuwa wanakabiliwa nao.

Alisema kwa mwaka wafanyabiashara wadogo walikuwa wanalipa ushuru wa zaidi ya Sh. 150,000, lakini hivi sasa baada ya kupata vitambulisho kwa Sh. 20,000, wafanyabiashara wameweza kutunza fedha zao na kufanya biashara bila vikwazo.



Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa (kushoto), akikabidhi zawadi kwa Nahodha wa Kivuko cha Mv. Magogoni, Abdul Ramadhani, kinachovusha wasafiri waendao Kigamboni na Feri, jijini Dar es Salaam, jana, kutokana na utendaji kazi wake, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 20 ya kampuni hiyo nchini. Kampuni hiyo, pia iliwalipia nauli ya kivuko wateja 6,000. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miradi 7,000 yafanyiwa EIA ndani miaka 5

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeainisha mafanikio lukuki yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano ikiwamo ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kwa miradi zaidi 7,000.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi, na kubainisha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano NEMC imeweza kufanya EIA katika miradi zaidi ya 7,000 pamoja na kutoa vyeti vya mazingira kwa miradi 3,500.

"Kwa kipindi cha miaka mitano kama baraza tumefanikiwa mambo mengi ambayo yamekuwa na manufaa makubwa katika kuchangia maendeleo na ukuaji wa uchumi. Idadi ya utoaji wa vyeti vya mazingira na idadi ya miradi iliyofanyiwa EIA imeongezeka mara dufu," alisema.

Amesema baraza litaendelea kuchukua hatua katika kukabiliana na changamoto za mazingira katika upande wa utupaji wa taka hatarishi na kudhibiti utiririshaji wa kemikali zenye sumu katika maeneo ya migodi.

"Katika eneo ambalo limekuwa na changamoto kubwa ni utupaji wa taka hatarishi, tumeendelea kuchukua hatua mbalimbali kudhibiti tatizo hilo kwa kuwa huleta athari za kudumu kwa maisha ya watu na viumbe hai vingine," alisema na kuongeza kuwa NEMC imetoa vibali 151 kati ya maombi 481 ya ukusanyaji wa taka hatarishi yaliyowasilishwa.

Alisema NEMC imesimamia utupaji wa tani 2,493 na lita 2,480 za taka hatarishi zilizokwisha muda wake na kufanya ukaguzi katika miradi 15,000 ambavyo vina vyeti vya EIA.

"NEMC mbali ya kusimamia utupaji wa taka hatarishi tani 2,493 pamoja na lita 2,480 ambazo ni kemikali za dawa zilizoisha muda wake, tumefuatilia kwa ukaribu miradi saba mikubwa ya madini hapa nchini kwa lengo la kupunguza au kuzuia kabisa visa vya uchafuzi wa mazingira," alisema.

Dk. Gwamaka alieleza kwamba mpaka baraza limepokea na kushughulikia kero 4,567 zinazohusiana na uchafuzi mazingira wa hewa, maji na ardhi.

# Mkakati waendelea kuwaendeleza makandarasi wazalendo

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Makandarasi nchini (CRB), imepanga kufanya mwendelezo wa mikutano ya kanda na makandarasi wazalendo ikiwa ni mkakati wake wa kuwajengea uwezo makandarasi hao ili waongeze ufanisi katika kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Msajili wa Bodi hiyo, Rhoben Nkori, wakati akifunga mafunzo ya siku moja kwa makandarasi hao.

Mafunzo hayo yalihusu namna makandarasi wazalendo wanavyoweza kuungana na kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu na namna bora ya kulipa kodi kwa Mamlaka ya Mapato (TRA).

"Bodi inaona umuhimu wa kwenda tena kwenye kanda zetu na kufanya mikutano ya mwaka ambayo ni minne itakayofanyika Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam na itaanzia Machi mwakani na itaishia Mei, ambapo mkutano wa mwisho wa kilele utafanyika Dar es Salaam," alisema Nkori.

Alisema makandarasi wengi wa Tanzania ni wadogo wadogo wakati makandarasi wa nje ni wachache, lakini wanatekeleza miradi mikubwa, hivyo wanawapa mafunzo ya kuungana ili wafanye miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu.

"Makandarasi wanauwezo tofauti wapo wenye uwezo wa kifedha, wenye uwezo wa kimitambo na wako ambao ni wataalamu zaidi kwenye fani, hivyo wakiunganisha nguvu zao wanaweza kufanya miradi mikubwa kwa wakati na kwa viwango bora zaidi," alisema.

Mkandarasi Christopher Nyagaswa ambaye ni mkurugenzi wa kampuni ya Ostrich, alisifu mkakati wa bodi hiyo kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo kupitia mafunzo hayo, ili waweze kushindana na wenzao wa nje.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa yakiwasaidia makandarasi kuongeza ufahamu kuhusu mambo mbalimbali ya namna bora ya kulipa kodi kwa mamlaka ya mapato na umuhimu wa kuungana.


"Mkandarasi mzoefu ambaye ameshiriki kwenye kazi za ubia kwa muda mrefu ametupa uzoefu wa namna ya kuungana, changamoto zake na tahadhari kuingia kwenye ubia ambao unaweza usiwe na manufaa, tunaomba muda wa mafunzo," alisema.

Nyagaswa aliiomba CRB kuendelea kutoa mafunzo ya aina hiyo kwenye kanda zote nchini, ili kuwafikia makandarasi wengi wazalendo na kuwajengea uwezo wa kushindana kwenye zabuni kubwa.

Alisema makandarasi wazalendo wanakabiliwa na changamoto ya mitaji ikiwamo masharti magumu ya ukopaji kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi.

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI OKTOBA 29, 2020





Ukurasa 12

**Mtu kujichora 'tatoo' kunazuia maabara kubaini kansa mwilini**



Ukurasa 13

**Operesheni kung'oa robo ya udumavu wa watoto wapatikanao Mkoa wa Pwani**

# MDIMNI: Kijiji kinachohama kukwepa mabadiliko ya tabianchi wanakoishi

- Maji yasogea km. 1, chanzo kina bahari
- Imetimua watu 400 kuelekea vijiji jirani

**Na Jenifer Gilla, ALIYEKUWA MKURANGA**

NI umbali kilomita 110 kutoka jijini Dar es Salaam, kunakopatikana kijiji cha Mdimni, Wilaya ya Mkuranga, mkoa Pwani, ambako wakazi wake kiuchumi wanategemea uvuvi na kilimo cha mazao ya korosho, mpunga na mahindi.

Mtu anapofika kijijini akitokea upande Kusini, atavutiwa na mandhari yaliyopambwa na nyumba za udongo zilizoezekwa na makuti, zikiwa katika mpangilio wa mistari miwili iliyonyooka na kuacha barabara kubwa katikati, inayopafanya kuwa na taswira ya kipekee.

Ukarimu wa wakazi nao unaonyesha ni wapenda ugeni wanaohudumia kila walichojaliwa nacho, pasipo kujali dhamira ya ugeni na si rahisi kutambua mzigo mzito wa hofu ya mazingira wanaobeba mioyoni mwao.

Kaskazini, wamepakana na Bahari ya Hindi, ambayo ndio inatajwa kuwa jinamizi linawakosesha usingizi hata wakawa wahamaji maarufu kwa miaka 17 sasa.

**SIMULIZI ZAO**

Ni wanakijiji wanaohama kukimbilia Kusini, wakipisha maji ya bahari yanayovamia makazi, kutokana na kina chake kuongezeka kadri siku zinavyosogea.

Mzee Selemani (65), mkazi wa kijiji hicho anasimulia mkasa wa kuponea chupuchupu kufa maji usiku wa manane, baada ya wimbi la maji ya bahari kuvunja ukuta wa nyumba yao na kuingia ndani.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Mdimni, Kadam Ulaga, akiwa eneo la kijiji ambacho wakazi wengi wamehama kutokana na kuvamiwa na maji ya bahari. **PICHA: JENIFER GILLA.**

"Nakumbuka ilikuwa mwaka 2003 siku ya Jumamosi, tulikuwa tunajiandaa kuhama, lakini kwa kuwa nyumba yetu huku juu ilikuwa bado haiajaezekwa, tukaona tuvutevute kidogo.

"Hiyo siku tumelala usiku, likaja wimbi kubwa na kubomoa ukuta kwa chini, sisi hatuna habari kumbe maji yalikuwa yanaingia kwa nchini.

"Tuliokolewa na mtoto wangu ambaye alikuwa na miaka saba, alikuwa anaamka kwenda msalani ndipo akaona maji yanaingia ndani kwa kasi, akapiga kelele tukaamka nyumba nzima," anasimulia mkasa,

Mzee huyo anawakilisha jumla ya wakazi 1,390 wanaoishi kijijini, ambao kila mmoja ana lake lililomkuta kutokana na adha hiyo.

Mwenye simulizi mwingine ni mvuvi Latifa Mbonde, anayesimulia kulazimika kufanya shughuli hiyo, baada ya eka 10 walizokuwa wanalima mpunga na familia yake, kuvamiwa na maji ya bahari.

Anakumbuka, walivuna gunia zisizopungua 50 za mpunga kila mwaka kutoka shambani hapo baada ya mauzo walipata Sh.milioni mbili kila mwaka, ili tomkimu na watoto wake

" Tulikuwa na maisha mazuri hatukuwa na shida, tulifanikiwa kujenga nyumba kubwa, lakini mwaka 2005 mambo yalibadilika na sisi maji yakatufikia kwenye shamba letu tukiwa na mali shambani.

"Hatukuweza kuvuna kwa kuwa mpunga ulikuwa bado mbichi, hivyo ekari 10 zote zilikufa," anaeleza Latifa, huku akilengwa na machozi.

Mama huyo mwenye umri miaka 50, anasimulia ndipo namna alivyoingia rasmi kwenye uvuvi mwaka 2009, baada mume wake kufariki na maisha yakamwia magumu.

Anasema kutokana mbinu duni za uvuvi anazotumia, anaishia kuambulia wastani Sh.5000 kwa siku na inaelezwa ni waliopata hasara ya maisha na namna hiyo wakaendelea na shughuli hiyo katika maeneo mengine kama kilimo.

Diba Kisagulu, ana simulizi alivyohama eneo Bonde la Ndege mwaka 2003, baada ya eneo la hekari 5 walikuwa wakilima mtama na mpunga kuvamiwa na maji ya bahari hivyo udongo kukosa rutuba ya kuendelea na kilimo.

Anasimulia alipata eneo sehemu ya juu katika kijiji hicho ambako ni shamba la mikorosho lililomilikiwa na baba yake kwa muda mrefu.

"Kwa hiyo, imekuwa kama bahati. Nashukuru sasa nalima mahindi na korosho ndio tunapata kula, ila hofu yangu ni haya maji yakifika huku tuliko nitakwenda wapi", analalama Diba.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Kadam Saidi, ni Mwenyekiti wa Kijiji hicho anayesema maisha yao yamejaa hofu kutojua hatima yao,

Endelea Uk. 14

# Matokeo ya awali yaanza kutoka




Mawakala wa vyama vyote wakihesabu kura za wagombea katika kituo cha Ukonga Mazizini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Waandishi Wetu**

MATOKEO ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani uliofanyika jana nchini kote, yameanza kutangazwa katika baadhi ya vituo.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, mkoani Dodoma katika Jimbo la Dodoma Mjini, mgombea urais wa CCM, John Magufuli anaongoza katika kura za urais huku mgombea wa ubunge kupitia chama hicho, Anthony Mavunde, naye akivuna kura nyingi.

**Kata ya Viwandani:**

**Kituo cha Ofisi ya VEO 2** nafasi ya ubunge Mavunde wa CCM (72), Aisha Madoga (CHADEMA) kura (nane). Kituo cha Ofisi ya WEO 2, Mavunde (59), Madoga (10).

Kwa upande wa urais, Dk. Magufuli (59), Tundu Lissu wa CHADEMA kura 12.

**Kituo cha WEO 1:** Mavunde (50), Madoga (6) na Kituo cha MOKU Security, Mavunde (85), Madoga (17).

Matokeo ya Dk. Magufuli (85), Tundu Lissu 17 na Mutamwega Mganywa wa SAU kura moja.

**Jumba la Maendeleo;** Mavunde (94), Madoga 25 na udiwani Khalifan Kabwe wa CCM (84), Salma Mambo (CHADEMA) kura 32.

**Kituo cha LAPF-2** matokeo ya urais ni Dk. Magufuli (67), Lissu (21) na maganja Kulwa (NCCR- Mageuzi) kura moja. Ubunge Mavunde (67), Madoga (21).

Kituo cha LAPF-1 ubunge Mavunde (70), Madoga (28) na urais Dk. Magufuli (74) na Lissu kura 33. Udiwani Cosmas (90), Kutika (50) na Chima kura 6

**Kikuyu Kusini:**

**Wera Sekondari 1;** Urais Dk. Magufuli (120), Lissu (18), Benard Membe (ACT Wazalendo) kura moja, Leopold Mahona kura moja. Ubunge Mavunde (120) na Madoga (19). Nafasi ya udiwani: Cosmas (83), Kutika (41) na Chima kura 13.

**Wera Sekondari 2** (Mkalama), urais Dk. Magufuli (102), Lissu (12) na Seif Maalim (AAFP) kura moja na ubunge Mavunde (104) na Madoga (13).

**Udiwani;** Jostico Cosmas (ACT -Wazalendo) kura 69, Martin Kutika (CCM) kura 39, Elia Chima (CHADEMA) kura 12.

**Kituo cha Wera Sekondari 3 urais:** Magufuli (104), Lissu (tisa) Mahona (moja) na ubunge Mavunde (104), Madoga (11). Udiwani; Cosmas (77), Kutika (26), Elia Chima (nane) (CHADEMA) kura 8.

**Wera Sekondari 2:** Urais ni Dk. Magufuli (132) na Lissu (13) huku ubunge Mavunde (129), Madoga (14). Udiwani Cosmas (90), Kutika (50) na Chima (sita).

**Wera Sekondari 2**, urais Dk. Magufuli (132) na Lissu (13).

**Ofisi ya Mwenyekiti Mtaa Uhindini -2 Urais;** Dk. Magufuli (81), Lissu (23), Leopold Mahona moja na Queen Sendiga (NRA) kura moja. Ubunge; Mavunde (78) na Madoga (26).

**Kata ya Mkuhungu: Shule ya Msingi Nkuhungu Na.1:** Urais Dk. Magufuli (129), Hashimu Rungwe (CHAUMA) moja na Lissu 34. Ubunge Mavunde (132), Madoga (32) na udiwani Jackson Majaliwa (ACT-Wazalendo) moja, Daudi Mkhandi (120), Vicent Emmanuel (40), Salum Nasibu (CUF) kura moja.

**Shule ya Msingi Nkuhungu Na. 2 Urais Dk. Magufuli 123**, Lissu 35 na Ubunge, Mavunde 127, Madoga 31.

**Shule ya Msingi Nkuhungu Na. 3 Urais Dk. Magufuli (119),** Lissu (19) na Ubunge Mavunde (117), Madoga (20).

Ofisi ya Mtendaji Mtaa Namba moja, Urais; Magufuli (122) na Lissu (18) na ubunge, Mavunde (120) na Madoga (19).

**Ofisi ya Mtendaji Mtaa Namba 3**, Magufuli (109) na Lissu (23), wakati nafasi ya ubunge Mavunde (112) na Madoga (19).

**Kata ya Uhuru Kituo cha Kipande -2** Ubunge Mavunde (65) na Madoga 27 na Kipande-1, Mavunde (CCM) 62 na Madoga (CHADEMA) 20.

**Kata ya Kizota Kituo cha Sekondari ya Kizota No.4** Urais Magufuli (61), Lissu (16) na ubunge ni Mavunde (63) na Madoga 14.

**Salama Na.3** Urais Magufuli (89) na Lissu (22) huku ubunge Mavunde (95) na Madoga (16).

**Kata ya Chang'ombe Kituo cha Msamaria-2;** Urais Magufuli (82), Lissu (16), Maganja (1), Mgahywa (1). Ubunge Mavunde (78), Madoga (20).

**Msamaria-4** Urais Magufuli (92), Lissu (13) na ubunge Mavunde (97), Madoga (7). Msamaria -3; Urais Magufuli (75), Lissu (23), Hashim Rungwe (CHAUMMA)-1 ubunge Mavunde (78), Madoga (21).

**Chang'ombe Juu B-1,** Urais Magufuli (56), Lissu (11), Ubunge Mavunde (59), Madoga (7)

**Kituo cha Msamaria-1** Urais Magufuli (87), Lissu (13), Membe (1) na Ubunge Mavunde (78), Madoga (24)

**DAR ES SALAAM**
**Jimbo la Temeke**

**Kituo cha Maganga B2:** Urais Magufuli (67), Lissu (17), Bernard Membe (1), Ibrahim Lipumba (3) na Queen Sendige (sita). Ubunge Doroth Kilave (CCM) 63, Sina Manzi (CHADEMA) saba, Zainabu Amir (CUF) 12, Yahaya Mapanda (ACT-Wazalendo) mbili.

**Usalama Na. 2,** Urais Dk. Magufuli (86), Lissu (17), John Shibuda (2) na Lipumba (2).

Kwa nafasi ya ubunge, Kilave (75), Zainabu Amir (CUF) kura tisa, Sina Manzi (CHADEMA) kura 8, Zainabu Kilindo (AAFP) kura tano, Yahaya Mpanda (ACT) kura tano, Khamis Kimwaga (TADEA) kura mbili na Shaban Chumu (Demokrasia Makini) kura moja.

**Maganga B2,** nafasi ya urais Magufuli (67), Lissu (17), Membe (1), Prof. Lipumba (3) na Sendiga (6) wakati ubunge ni Kilave (63), Manzi (7), Amir (12) na Mapanda (2).

**Segerea**

Ofisi ya Madenge B.1 Buguruni, Dk. Magufuli (62) na Lissu (19), Membe (2), Lipumba (1) na Mahona moja. Kwa ubunge Bona Kamoli wa CCM (52), Maharagande Mbarali (ACT- Wazalendo) 17, Mrema Edward (CHADEMA) tisa na Sabreena Sungura (CUF) tano.

**Kituo cha Madenge A-6;** Urais Magufuli (59), Lipumba (2), Membe (3,) Rungwe (1) na Lissu (10) wakati ubunge ni Kamoli ( 50), Sungura (6), Mrema (9) Maharagande (4), Heristus Ndali (CCK) moja.

**Kituo cha Madenge A-6** Buguruni, Urais: Magufuli (59), Lipumba (2), Membe (3), Rungwe (1) na Lissu (10). Ubunge Kamoli (50), Sungura (6), Mrema (9), Maharagande (4), Ndali kura moja.

**Kituo Cha MEO Madenge B** (5) urais Magufuli (46), Lissu (24), Shibuda (1) na Membe (2).

**Buguruni Madenge B-4,** Magufuli (55), Lissu (20), Lipumba (2), Membe (2) na Ubunge Kamoli (50), Mrema (11), Sungura (4) na Maharagande (13)

**Ilala**

**Ofisi ya Mtendaji Amana 2; urais:** Magufuli (62) na Lissu (33), ubunge: Mussa Azzan Zungu (CCM) kura 61, Hashim Issak (CHADEMA) 28, Hussein Abdallah (ACT- Wazalendo) tatu, Abdallah Kabara (CHAUMMA) moja na Clinton Jovin (NCCR) moja

**Ofisi ya Mtendaji Amana 4,** Urais: Magufuli (46), Lissu (37), Maganja Kulwa (moja), Rungwe (2). Membe (moja) na Lipumba moja.

Katika nafasi ya ubunge Zungu (46), Issak (29), Amina A.A (SAU) moja, Hussein J.A sita, Rashid (mbili) na Clinton (tatu).

**MWANZA**
**Ilemela**

Matokeo yaliyobandikwa kwenye **Kituo cha Mabomba Manne**, Jimbo la Ilemela, katika vituo vidogo, yalionyesha Dk. Magufuli (81), Lissu (33); Dk. Magufuli (80) Lissu (30); Dk. Magufuli (65), Lissu (40); Dk. Magufuli (86), Lissu (35); Dk. Magufuli (76), Lissu (42).

Kwa upande wa ubunge, matokeo katika vituo vidogo yalionyesha Dk. Angelina Mabula (CCM) kura 76, Grayson Warioba (CHADEMA) kura 34; Dk. Mabula (69), Warioba (37); Dk. Mabula (60), Warioba (40); Dk. Mabula (83), Warioba (36); Dk. Mabula (67), Warioba (47).

**Nyamagana**

**Matokeo kwenye kituo cha Ofisi ya Kata ya Isamilo A** yalionyesha Dk. Magufuli (75), Lissu (32); Dk. Magufuli (87), Lissu (16).

**SHINYANGA:**
**Kahama Mjini:**

**Katika kituo cha Shule ya Msingi Nyahanga A,** matokeo yaliyobandikwa jana yalionyesha Dk. Magufuli (83), Lissu (36) na Mutamwega Mgahwya wa SAU alipata kura moja.

Kwa nafasi ya ubunge yalionyesha Jumanne Kishimba (CCM) kura 69, Thadeo Mwati (CHADEMA) kura 48 na Hosea Paul (CUF) kura moja.

**Shinyanga Mjini**

Kituo cha Bugoyi, Kata ya Ndembezi, Ubunge Patrobas Katambi (CCM) kura 49, Salome Makamba (CHADEMA) kura 35. Kwa nafasi ya urais Dk. Magufuli kura 60 na Lissu kura 31.

Kwenye Kituo cha Mihale Jomu, Kata ya Kambarage ubunge Godwin Makomba (ACT) kura moja, Katambi (46), Makamba (39) na urais Dk. Magufuli

(58) na Lissu kura 26.

**KATAVI**
**Mpanda Mjini**

Shule ya Sekondari Mwangaza (Na. 1), matokeo yalionyesha Dk. Magufuli (70), Lissu (26) huku kura za ubunge zikionyesha 54 kwa Rhoda Kunchela wa CHADEMA na 43 kwa Kapufi wa CCM.

**KILIMANJARO**
**Moshi Mjini**

**Katika Kata ya Kiusa ubunge,** Buni Ramole (ACT-Wazalendo) kura 2, Priscus Tarimo (CCM) kura 64 na Raymond Mboya (CHADEMA kura 8. Nafasi ya Urais, Magufuli (73), Lissu (74) na Prof. Lipumba (1).

Kituo cha Ofisi ya Kata ya Kiusa J, urais Lissu (77), Dk. Magufuli (74), Kiusa 1 Dk. Magufuli (76) na Lissu (71).

**ARUSHA**
**Arusha Mjini**

**Kata ya Themi kituo cha Zahanati A,** urais Dk. Magufuli (96), Lissu (37) na ubunge Mrisho Gambo (CCM) 88, Godbless Lema (CHADEMA) (44.

**Kituo B:** Urais Dk. Magufuli (91), Lissu (47). Ubunge: Gambo (87), Lema (48). Kituo urais Dk. Magufuli (89), Lissu (41) na ubunge Gambo 83, Lema 43. Kituo D: Dk. Magufuli (100), Lissu (36). Ubunge: Gambo (94), Lema (40). Kituo E: Magufuli (86), Lissu (36). Ubunge: Gambo (72), Lema (48).

***Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA), Beatrice Shayo, Mary Geofrey, Beatrice Moses, Christina Mwakangale (DAR), Mary Mosha (MOSHI), Marco Maduhu na Shabani Njia (SHINYWNGA), Issack Allan (ARUSHA), Richard Makore (Mwanza), Neema Hussein (KATAVI), Nebart Msokwa na Grace Mwakalinga (MBEYA).***

AFYA

# Operesheni kung'oa robo ya udumavu wa watoto wapatikanao mkoa wa Pwani

## •Kitaifa yang'ang'ania theluthi moja

**Na Julieth Mkireri, Kibaha**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linaueleza utapiamlo kuwa upungufu, ziada au kukosekana usawa katika kiwango cha chakula kinachompa mtu nguvu au virutubisho mwilini.

Ni hali inayotokea kwenye makundi mawili; kwanza kutokuwa na lishe ya kutosha inayojumuisha kudumaa, kuwa na uzito mdogo pamoja na kukosa virutubisho vya kutosha.

Pili, inatajwa kuwa mlo unaoleta unene uliopitiliza, magonjwa na mtindo wa maisha, hali inayowapata zaidi watoto na wenye kipato kikubwa na hasa waishio mjini.

Kimsigi, mwanadamu uwezo wake umegawanyika katika makundi makuu matatu; protini inayojenga mwili, mlo wa kulinda mwili na unaotia nguvu kutoka jamii ya wanga.

Sababu ya watoto kupata utapiamlo unaosababisha udumavu wa akili na mwili, ni kwamba familia nyingi hula vyakula vya wanga zaidi kama vile ugali wa mahindi, unga wa mtama, muhogo, mchele na vyakula jamii ya maharage.

Milo mingi inaelezwa kitaalamu imekosa mchanganyiko wa protini kutoka kwa wanyama, mimea, mboga na matunda.

Ripoti ya ya Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) inayoangalia viwango vya ukosefu wa lishe kati ya mwaka 1992 hadi 2015, inaonyesha udumavu na utapiamlo sugu umepungua kutoka asilimia 50 hadi 34 kw a wakati huo.

Pia, utapiamalo uliokithiri nao unapungua kutoka asilimia saba hadi tano na hali ya upungufu wa uzito ikipungua kutoka asilimia 24 hadi 14.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ana ufafanuzi kwamba, imeendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji chakula, dawa na vifaa vya kupima hali ya lishe na kujengea uwezo wa watoa huduma.

"Katika kupambana na utapiamlo nchini, wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Lishe imetoa matone ya nyongeza ya Vitamin A kwa watoto wa kati ya miezi sita na miaka mitano sambamba na dawa za minyoo kwa watoto wa umri kati ya mwaka mmoja na miaka mitano," anaeleza.

Kitaalamu, mpaka mwanadamu anapofikisha siku 1000, kinatajwa kuwa kipindi muhimu kinachoamua maisha yake katika uwezo binafsi, ikiwamo wa kufikiri.

**MAPYA YANAYOJIRI**

"Elimu ya lishe bora inahitajika kwa wazazi, wanafunzi na walimu katika mapambano ya kutokomeza hali ya udumavu katika Halmashauri yetu ya Mji wa Kibaha," anasema Aisha Yusuph, mkazi wa Maili Moja, Kibaha.



Watoto wakiwa na mama zao katika matukio ya kijamii. Lishe na matunzo bora, ni silaha muhimu kwao kimaisha, zinazooneka kwenye tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Huyo ni mkazi wa Maili Moja, anayesema ni vyema elimu ikawafikia walengwa ambao ni watoto na walezi wao waliopo nyumbani na shuleni, wakatokomeza hayo, wanafunzi wakiwa katika afya njema,

Anasema, kuna wazazi wasipoata mlo bora ndani ya familia zao, hata kuwaathiri watoto walioko shuleni wasipate chakula, hivyo ana msisitizo kwamba, elimu ya lishe inatakiwa kuanzia shuleni na nyumbani, ili watoto wanapofundishwa wawe katika afya nzuri na ufaulu ukaongezeka.

Anafafanua: "Ishirikishwe kuwezesha watoto wetu kupata mlo wakiwa shuleni, pia kwa wale ambao wanaoshindwa kuchangia, kutokana na hali zao tuombe serikali itusaidie"

Pia, udumavu asili yake unatajwa unatokana na utapiamlo unaosababishwa na mtoto kukosa lishe bora kwa kipindi cha muda mfupi na moja ya dalili zake ni mtoto kuwa na mfupi, akilinganishwa na umri wake.

Kuna sababu zinazoangukia mahsusi kwa baadhi ya familia ndani ya Halmashauri ya Mji Kibaha, inatokana na watoto kulelewa na bibi zao, ambao baadhi wako katika maisha duni.

Mgombea mmojawapo katika kura zilizopigwa jana jimbo la Kibaha Mjini, ana ahadi kwamba akipata ridhaa ya wapiga kura, atahakikisha elimu inatolewa kwa walezi wa watoto kuanzia umri chini ya miaka mitano.

Mwanasiasa huyo anaeleza kwamba ni elimu itakayosaidia kundi la walezi kuwaongoza namna ya kupata na kula lishe bora, ili kuondokana na udumavu.

Inabainishwa, elimu ya ujasiriamali na kuwahamasisha wananchi kujiunga na vikundi vya ujasiriamali ni muhimu, ili wakopesheke na hata kunufaika na mikopo itakayowaondoa katika mazingira duni, wamudu kupata vyakula bora

Mji wa Kibaha, uliomo katika orodha ya halmashauri tisa za mkoa wa Pwani, una jumla ya wakazi 157,695, ndani yake wako watoto 19,879 walio na umri chini ya miaka mitano.

Ofisa Uhusiano wa Halmashauri ya Mji Kibaha Innocent Byarugaba, anaeleza kuwa halmashauri hiyo ilianza kutekeleza mkataba wa lishe, kuanzia Januari 2018 na katika ngazi ya kata ilianza Agosti 2019.

Byarugaba anasema, udumavu katika halmashauri kwa sasa uko asilimia 0.02 na mikakati inaendelea kuutokomeza.

Anafafanua kuwa, katika shule za msingi ni madarasa ya mitihani pekee yanayopata chakula shuleni, katika makubaliano ya wazazi na kamati za shule kuwawezesha watoto waendelea na masomo muda wa mchana.

Kinachofafanuliwa hapo ni kwamba, hakuna mzazi anayelazimishwa kuchangia chakula shuleni, kwa kuwa baadhi yao wana hali duni zao kiuchumi ni duni zaidi na kamati za shule ndizo zinazohusika kwa kushirikiana na wazazi na walezi wanaokubaliana na utaratibu huo

Anasema, halmashauri inatekeleza shughuli za lishe ikiwamo ukaguzi wa maduka ya vyakula na viwanda vinavyotengeneza, mafunzo elekezi kuhusiana na masuala lishe yanatolewa kwa watoa huduma vituoni na majumbani

"Halmashauri imekuwa ikitoa elimu kwenye shule zilizopo, pia upimaji wa madini joto na utoaji elimu wa madini hayo," anasema.

Kwa mujibu wa B yarugaba, wameshafanikiwa kutoa elimu kwa huduma za mkataba na kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kisha wakajumuisha shughuli za lishe katika Idara ya Elimu, Kilimo na Mifugo.

Akijadilli kuhusu mikakati ya Halmashauri hiyo, Byarugaba anasema mojawapo ni kutoa elimu ya lishe kwa vijana waliopevuka shuleni, kwa kuanzisha siku ya afya na lishe mitaani.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Injinia Evarist Ndikilo, alifanya kikao na wakuu wa wilaya na kutoa agizo kila mmoja kusimamia kikamilifu suala la lishe bora katika wilaya zao, kauli aliyotoa

Katika Kikao Cha pili Cha Tathmini ya Mkataba wa Lishe kwa kipindi cha Januari hadi Juni iliyopita.

Injinia Nduikilo, anawataka wakuu wa Wilaya kutumia wataalamu wa afya kuelimisha wananchi kuhusu lishe bora itakayoambatana na uhamasishaji watoto kupata chakula shuleni.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa tatizo la udumavu kitaifa ni asilimia 31 na mkoa huo umefikia asilimia 23.=



MAZINGIRA

# MDIMNI: Kijiji kinachohama kukwepa mabadiliko ya tabianchi wanakoishi

INATOKA UK.11

kwa kuwa kila baada ya muda wanalazimika kusogea juu kukimbia mafuriko kutoka baharini.

Anesema, mpaka sasa wameshahama karibuni kilomita mbili kutoka makazi yao ya awali na kuacha takribani hekta 2000 za ardhi walizotumia kwa kilimo awali.

"Miaka ya 1990, wazazi wetu walikuwa wanaishi kulee(anaonyesha kwa mkono)!...hivi sasa hivi tunapaita Jangwa la Ndege, kwa sababu ni makazi ya ndege zimebaki nyumba chache wanazoishi wavuvi ambazo nazo zimeshafikiwa na maji.

"Kutokana na kuvamiwa na maji ya bahari, tukawa tunasogea kidogo kidogo mpaka tumefika hapa unapotuona," anaeleza mwenyekiti kwa uchungu.

"Mpaka tunafika hapa tumeshapoteza takribani heka 2000 ambazo tulikuwa tunazitumia kwa kilimo cha mpunga na ufuta. Eka 1,500 zimejaa maji ya chumvi na heka 500 zimepatwa na mmomonyoko, hivyo pamekuwa jangwa tu," anasema Saidi.

Akiwa mzazi mwenye familia ya watoto watatu, anasema mwezi tarehe 13 hadi 16 na mwisho wa mwezi, tarehe 26 hadi 30, eneo hilo linajaa maji ya hali inayofanya wapite kwa shida wakielekea kwenye shughuli za uvuvi.

Mwenyekiti wa kijiji huyo anasema, sensa waliofanya mwaka jana na kuonyesha kuwapo wengi wamehamia kijiji cha Kisemvule ambapo wanafanya kazi za viwandani.

Ramadhani Saidi ni mkazi wa Kijiji cha Mdimni aliyehamia eneo la Kisemvule ambaye ana haya ya kueleza:

"Nimehamia huku mwaka 2014 baada ya maisha kuwa magumu hapo kijijini, tangu tumehama kule kwenye maeneo yetu yaliyovamiwa na maji na kuja huko juu maisha yamekuwa magumu, hatuna maeneo kulima, samaki nao wamekuwa adimu kuvua, nimeona nihamie huku na familia tuangalie upepo" anasema.

Kwa mujibu wa Ramadhani kama mambo huko kijijini mdini yatakuwa mazuri, kuna jopo tayari kurudi na uendelea na biashara ya samaki kwa kuwa huko alipo maisha ni magumu kwa kuwa anategemea msharaha ambao ni mdogo.

**KUTOKA SERIKALINI**

Mkuu wa Wilaya Mkuranga, Philiberto Sanga, anasema serikali ilishaagiza wanakijiji hao kuhama katika eneo hilo kuepusha maafa na watafute mazingira mbadala yenye nafuu, mpaka watakapopata suluhisho la kudumu.

"Tumewaagiza wanakijiji kutafuta maeneo yanayofaa na kuhamia huko wakati tunafanyia kazi changamoto hiyo." Anaeleza Sanga.

Kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira(NEMC), Meneja wa Maeneo Maalum Yaliyoathirika na Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi, Fredrick Mulinga, anasema hawakuwa na taarifa za athari katika eneo hilo.

Huku akiahidi hatua kuchukuliwa haraka, Mulinga anasema wangepata taarifa hizo mapema kutoka wilayani wangeijumuisha kwenye taratibu za kutafutia fungu la pesa za kufanya kazi majanga hayo.

"Tumeingia mkataba na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCC), mfuko wao wa kusaidia kuhimili mabadiliko ya tabia nchi 'Adaptation Fund' huwa tunapokea pesa kwa ajili ya kusaidia maeneo yalioathirika." anasema na kuongeza:

"Kwa Dar es Salaam tulitumia dola milioni 50 kujenga ukuta wa maeneo ya (daraja) salender. Tutalifanyia kazi, tutakwenda kutembelea eneo hilo kisha tuone jinsi ya kulisaidia, ipo mifuko mingi inayosaidia majanga hayo kama vile Green Climate Fund, tunaweza kufanya kitu."

**WADAU NA YAO**

Salum Kigungo ni Makamu Mwenyekiti wa taasisi binafsi inayopambana na athari za mabadiliko ya tabianchi, iitwayo TCCI-Mazingira, anasema anakisaidia kijiji cha Mdimni kwa kuibua changamoto walio nayo, ijulikane kwa umma.

Pia, anasema wanatoa elimu ya kupandaji na kutunza miti na hasa ya mikoko, ambayo kwa kiasi kikubwa inadhibiti athari zinazotokana na kujaa maji ya bahari kwenye makazi ya watu.

"Tunaanzisha kituo cha upandaji miti hii ya mikoko (A Mangroves nursery) ambayo itasaidia sana kwenye uhifadhi wa mazingira ya eneo hilo." anasema Salum.

Ripoti ya Shirika la Kimataifa Linaloshughulika na Wahamiaji (IOM), inakubaliana na utabiri uliotolewa Jopo la Serikali za Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC) mwaka 1990, kuwa ifikapo mwaka 2020 kutakuwapo wahamiaji milioni 200 duniani.

Inataja chanzo kikuu kuwa ni wahamaji kuwa ni athari za mabadiliko ya hali ya hewa ikiwamo mmomonyoko wa udongo, kuathirika shughuli za kilimo na mafuriko yanatokanayo na kuongezeka kimo cha bahari.

Ripoti ya pili kutoka IPCC mwaka 2007, inakadiria kuwa nchi Kuisini mwa Jangwa la Sahara( Tanzania ikiwamo) mavuno ya mazao ya kilimo kinachotegemea mvua, yanaweza kushuka hadi asilimia 50 ifikapo mwaka huu.



Mwenyekiti wa kijiji cha Mdimni, Kadam Ulaga (katikati), akiwa na wazee wa kijiji hicho wakionyesha eneo la ekari 2000 walilotumia kwa kilimo, ambalo sasa limevamiwa na maji ya bahari. Chini, eneo lingine liloharibiwa. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA.**

**"Nimehamia huku mwaka 2014 baada ya maisha kuwa magumu hapo kijijini, tangu tumehama kule kwenye maeneo yetu yaliyovamiwa na maji na kuja huko juu maisha yamekuwa magumu, hatuna maeneo kulima, samaki nao wamekuwa adimu kuvua, nimeona nihamie huku na familia tuangalie upepo" anasema.**





# Wataalamu wa afya ya mazingira waitwa usajili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATAALAMU wa afya ya mazingira nchini wametakiwa kujitokeza kujisajili na kuhuisha leseni zao ili kutambulika na kufanya kazi zao kwa weledi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Eliud Elikaim, aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la Mazingira la awamu ya nne, jijini hapa.

Alibainisha kuwa wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamefanikiwa kuhuisha mwongozo wa maadili na nidhamu kwa watumishi wa umma.

Alisema mwongozo huo unataka kila baraza kuufuta ili kusimamia maadili na nidhamu za taaluma husika.

"Baraza la Afya ya Mazingita linatakiwa kuhakikisha wataalamu wote wa afya ya mazingira wakiwamo maofisa afya nchini kujitokeza kusajili na kuhuisha leseni zao, ili kusimamia vyema mazingira kwa kutoa mwongozo na kufanya usafi ili kuepukana na magonjwa ya milipuko yanayoweza kujitokeza," alisema.

Aidha, alilitaka baraza hilo kupitia upya sheria kwa kuangalia maeneo muhimu kwa ajili ya kufanya maboresho na kumshauri waziri ili kutengeneza kanuni chini ya Sheria ya Usajili sura ya 428.

Kwa upande wake, Msajili wa Baraza hilo, Iddi Hoyange, alisema baraza limetoa muda wa kusajili na kuhuisha leseni kwa wataalamu wa afya hadi mwezi Februari mwaka 2021.

Alisema mwezi huo utakuwa mwisho wa kujisajili hivyo wataalamu hao wasajili kabla ya kufika muda huo huku akisema baraza litaanza kufanya ukaguzi na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote watakaobainika kutotii wito huo.

**Mwezi huo utakuwa mwisho wa kujisajili hivyo wataalamu hao wasajili kabla ya kufika muda huo huku akisema baraza litaanza kufanya ukaguzi na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote watakaobainika kutotii wito huo.**

# EWURA mbioni kukamilisha mpango udhibiti majanga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mpango wa kupambana majanga yanayotokea kwenye njia za wazi za kupitishia miundombinu mbalimbali ikiwamo gesi, maji na umeme.

Hatua hiyo imetokana na ongezeko la ajali zinazotokana na kukosekana kwa udhibiti wa njia za miundombinu inayotumiwa na sekta za gesi, maji na umeme.

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema mpango huo utahusisha utungaji wa sheria na kanuni za udhibiti miundombinu chini ya ardhi hasa kunapofanyika matengenezo au ujenzi utakaohusisha uchimbaji maeneo yenye miundombinu.

Alibainisha kuwa tayari hati ya makubaliano ya kuwawezesha wadau wa miundombinu kuandaa mpango wa pamoja wa kulinda miundombinu hiyo imesainiwa.

**Baada ya kusaini makubaliano haya, kamati ya ufundi ya pamoja itaundwa ili kutengeneza kanuni za kisheria zinazoendana na makubaliano hayo.**

"Baada ya kusaini makubaliano haya, kamati ya ufundi ya pamoja itaundwa ili kutengeneza kanuni za kisheria zinazoendana na makubaliano hayo," alisema.

Alieleza kuwa EWURA itakuwa inafuatilia wadau namna wanavyofuata kanuni, taratibu na miongozo jambo litakalosaidia mamlaka kutoa haki, kwenye usuluhishi wa migogoro.

Aidha, alisema makubaliano hayo yatasaidia kuongeza usalama wa umma na mali zao, uadilifu na umadhubuti wa mfumo wa miundombinu ardhini kwa kuanzisha na kutumia miundombinu ya kisasa za kuzuia uharibifu wa miundombinu nchini.

Alitaja taasisi zilizotia saini makubaliano ni Kampuni ya Simu (TTCL), Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Pan African Energy (PAET), SONGAS na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC).

Nyingine ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Kampuni ya gesi ya Maurel & Prom, Wakala wa Barabara (TANROADS), Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) na Kampuni ya Bomba la Mafuta (TAZAMA Pipelines Limited).

Alieleza kuwa EWURA, TPDC na PAET mwaka 2018 zilijadiliana na kukubaliana kuchukua hatua za haraka kushirikisha wadau wote na wamiliki wa njia hizo, ili kutafuta namna ya kuwa na mfumo wa kudhibiti usalama wa miundombinu wakati ikikarabatiwa na ujenzi unaohusisha kuchimba.

"Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia ongezeko la ajali zinazotokana na kukosekana udhibiti wa njia hizo, mfano Aprili mwaka 2014 ilitokea ajali eneo la Kurasini Darajani, ambapo kampuni ya China Railway Construction Engineering Group (CRCEG) ilitoboa bomba la gesi wakati ikiendelea na shughuli zake," alisema.

Katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, mkurugenzi huyo alisema EWURA kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wadhibiti wa Marekani (NARUC) na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani (USAID) walikutana mwaka 2018 na kuitisha kikao kujadili uzito wa tatizo la usalama wa miundombinu na kukabiliana nalo.




Baadhi ya wakazi wa Chamwino Ikulu, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, wakiwa kwenye foleni kwa ajili ya kupiga kura ya uchaguzi mkuu kwenye kituo cha Idara ya Maji jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana wapewa neno usubiriaji matokeo

**Na Augusta Njoj,** DODOMA

KAMATI ya Amani ya Viongozi wa Dini Mkoa wa Dodoma, imewaasa vijana kutojihusisha na vitendo vyovyote vya uvunjifu wa amani wakati wakisubiri kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mkuu 2020.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Shekhe Mustapha Shabani, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa tamko la umoja wa viongozi wa dini kuhusu uchaguzi huo.

Alisema ni vyema Watanzania wakatunza amani kwenye uchaguzi huo na kuendelea kuliombea Taifa ili livuke salama.

"Sisi viongozi wa dini hatutarajii vurugu na maandamano, viashiria vya uvunjifu wa amani vinavyoweza kujitokeza wakati wa uchaguzi huu, Watanzania tuendelee kuwa watulivu na kuenzi amani ya Taifa ambayo ni tunu tuliyotunukiwa na Mungu," alisema.

Alibainisha kuwa jukumu la ulinzi wa amani ni la kila Mtanzania kwani endapo amani itapotea watakaoumia ni Watanzania wenyewe.

Aliwasihi vijana kutokubali kutumiwa na wanasiasa kwamba wabaki kwenye vituo, na kwamba wanatakiwa wakipiga kura warejee majumbani mwao, ili kusubiri matokeo kwa kuwa jukumu la kulinda kura ni mawakala wa vyama pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Sisi kama viongozi wa dini ni jukumu letu kukemea vitendo vya uvunjifu amani na kuhamasisha wananchi ambao ndio waumini wetu kuwa watulivu."

Alisisitiza wazazi na walezi kwenye kila familia kuwaasa vijana wao kujiepusha na kila aina ya vishawishi kwenda kuandamana na kufanya fujo kwa sababu mwisho wa siku watakabiliwa na sheria za nchi na wale waliokuwa wakiwahamasisha.





# Mbunge wa zamani akabidhi kituo cha polisi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

ALIYEKUWA Mbunge wa Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya, Haroon Pirmohmed, amejenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbarali na kukikabidhi serikali kwa ajili ya kuanza kutumika, huku akidai kuwa lengo lake ni kuimarisha ulinzi na usalama wilayani humo.

Alikabidhi kituo hicho mwishoni mwa wiki kisha kupokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila pamoja na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei ambaye alimwakilisha Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Haroon alisema kituo hicho kimejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 160 na kwamba eneo kilipojengwa ni sehemu ya shamba la kampuni yake ya Mbarali Estete na kwamba eneo hilo lina ukubwa wa ekari moja.

Alisema maeneo muhimu yaliyojengwa ni jengo lenye ofisi mbalimbali, choo, eneo la kuegesha magari pamoja na eneo maalumu kwa ajili ya maaskari kufanya mazoezi ya utimamu (kwata).

**Sisi kama serikali tunakushukuru sana mzee Haroon maana hiki kituo ni muhimu sana, nawaomba wananchi wa Mbarali hiki kituo msikizinduwe kwa kuswekwa humo kwa sababu ya fujo wakati huu wa uchaguzi.**

Alisema ujenzi wa kituo hicho ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi zake alizozitoa wakati alipokuwa anaomba kura kwa wananchi wakati wa uchaguzi mkuu wa 2015, aliahidi kukijenga ili kuimarisha ulinzi na usalama wilayani humo.

"Uchumi wa nchi unaimarika endapo kuna amani na utulivu wa kutosha, hivyo mimi pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Kapunga Estate tuliamua kujenga hiki kituo ili kuimarisha utulivu na watu wafanye kazi kwa amani," alisema Haroon.

Akipokea kituo hicho, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alimshukuru mbunge huyo wa zamani kwa ujenzi wa kituo hicho, akisema kuwa ni watu wachache ambao wanakuwa na moyo wa kujitolea hasa wanapokuwa wameachana na siasa.

Aliagiza Ofisi ya Ardhi ya Wilaya ya Mbarali kuliondoa eneo hilo kwenye hati ya shamba la mwekezaji huyo ili liandaliwe hati yake na lisiwe tena sehemu ya shamba hilo.

Chalamila alisema kituo hicho ni muhimu kwa ajili ya ulinzi kwenye eneo hilo kutokana na Mji wa Ubaruku kuwa na shughuli nyingi za uzalishaji pamoja na kituo cha mabasi cha Ubungo ambacho kipo jirani na kituo hicho.

"Sisi kama serikali tunakushukuru sana mzee Haroon maana hiki kituo ni muhimu sana, nawaomba wananchi wa Mbarali hiki kituo msikizinduwe kwa kuswekwa humo kwa sababu ya fujo wakati huu wa uchaguzi," alisema Chalamila.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Matei alisema kwenye mapokezi ya kituo hicho, IGP Sirro alitakiwa awepo, lakini alishindwa kufika kwa sababu alikuwa ametingwa na shughuli zingine za kitaifa hivyo alimwagiza amwakilishe.

Alisema kituo hicho kitawasaidia kwenye shughuli mbalimbali za ulinzi na usalama kwenye wilaya hiyo ambayo imekuwa na matukio mbalimbali ya uhalifu.

Aliwaomba wadau wengine kujitolea kuboresha miundombinu ya Polisi ili kuboresha huduma hiyo muhimu.



Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi 'Sugu', akiwa na mkewe Happiness (katikati), baada ya kupiga kura katika kituo cha Tonya, Kata ya Ilomba, jijini Mbeya, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Chalamila ataka amani, utulivu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaomba waimbaji wa nyimbo za injili, kuendelea kuimba nyimbo zenye kuhamasisha amani na utulivu kipindi hiki cha uchaguzi ambao Watanzania jana walichagua rais, wabunge na madiwani.

Chalamila aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao na wasanii wa nyimbo za injili kilichokuwa na lengo la kujadili namna kundi hilo litaweza kutumia sanaa yao kuhubiri amani katika mchakato mzima wa uchaguzi mkuu.

Alisema wakati huu ni muhimu kwa makundi ya sanaa kuhamasisha wananchi kulinda amani na utulivu baada ya kupiga kura na kusubiria matokeo.

Alitoa angalizo hilo baada ya kudai baadhi ya kauli za viongozi wa kisiasa kwamba ni wajibu kulinda kura vituoni.

"Ni wakati wa waimbaji kuimba nyimbo zenye kuhamasisha watu kuitunza amani na jukumu ni la kila Mtanzania, huku waimbaji mkiwa na wajibu huo kwa sababu ni rahisi ujumbe wenu kusambaa kwa haraka," alisema Chalamila.

Aliwaomba pia viongozi wa dini mbalimbali kutumia muda huu kuendelea kuliombea amani na utulivu taifa sambamba na kuwahamasisha waumini kutunza amani muda wote wa mchakato wa uchaguzi.

Mratibu wa Uchuguzi, Mwajabu Abdallah, alisema serikali iliatoa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi ikiwamo vya watu wenye ulemavu.

Kwa upande wake, Askofu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God Tanzania TAG, Jimbo la Kaskazini, Prof. Donald Mwanjoka, aliwaasa wakazi wa Mkoa wa Mbeya kutokubali kuingizwa kwenye vuguvugu la kuharibu uchaguzi kama vile maandamano au kuwafanyia vurugu wasimamizi wa uchaguzi.

# STAMICO yaagizwa mfumo wa kutambua miamba

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI imeliagiza Shirika la Madini la Taifa STAMICO, kuandaa mfumo wa kutambua miamba yenye mashapo ya madini na kufanya tathmini ya kiwango cha madini kilichopo ardhini.

Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, alitoa agizo hilo, wakati akizindua kiwanda cha mfano cha kuchenjua madini ambacho kimejengwa na serikali katika eneo la Itumbi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.7.

Nyongo alisema lengo la mkakati huo ni kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini kujifunza uchimbaji madini wa kisasa na kufahamu mahali sahihi pa kufanyia shughuli zao ili waachane na uchimbaji wa kubahatisha.

"Mara nyingi wachimbaji wanachimba kwa kubahatisha wengine wanaamua kuuza mali zao, ili kuwekeza kwenye uchimbaji sasa tunataka wajue namna ya kupata miamba au madini vituo hivi vitatumika kuwaelekeza namna bora ya kuchimba," alisema Nyongo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Saimon Msanjila, alisema serikali imejenga vituo vitatu vya aina hiyo nchini ambavyo vimegharimu jumla ya Sh. bilioni 4.7.

Alisema watahakikisha wanawasaidia wachimbaji wadogo nchini kujifunza teknolojia na mbinu za uchimbaji wa kisasa, ili kujikwamua kiuchumi.

Alidai vituo hivyo vitatu, vyote vimejengwa na kampuni ya Tan Discovery Mineral Consultance Company Limited ambayo imesema pia imeandaa teknolojia na mbinu za kisasa za uchimbaji wa madini ambazo wataanza kuzionyesha mwakani kwenye maadhimisho ya siku ya madini itakayofanyika mkoani Geita.

Baadhi ya wachimbaji madini wilayani humo, walipongeza hatua ya serikali kituo cha mfano cha kuchenjua madini kwa madai teknolojia hiyo ya kisasa itasaidia upatikanaji wa madini kwa urahisi na salama.



# Mgombea ADA-TADEA, Jecha wasifu uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar, kupitia Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, amesema uchaguzi mkuu umefanyika katika mazingira ya uwazi na kuipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Wakati mgombea huyo akisema hivyo, aliyekuwa Mwenyekiti wa ZEC katika uchaguzi mkuu uliopita, Jecha Salim Jecha, ameibuka na kupongeza mchakato unavyoendelea.

Khatib alisema jana kwamba wagombea wa vyama vyote wamekuwa wakishirikishwa kila hatua pamoja na mawakala wa vyama kupewa nafasi ya kutekeleza majukumu yao ya kusimamia kura za wagombea.

"Uchaguzi kwa mtazamo wangu umefanyika katika mazingira ya uwazi. Wagombea tumeshirikishwa kila hatua na uchaguzi unaendelea vizuri kama nilivyoshuhudia baada ya kutembelea vituo mbalimbali," alisema mgombea huyo baada ya kupiga kura katika kituo cha Kiembe Samaki wakati akizungumza na waandishi wa habari.

**Mimi niko tayari kupokea matokeo yoyote yale na niko tayari kufanya kazi na kumpa ushirikiano mgombea yeyote atayetangazwa kuwa Rais wa Zanzibar.**

Hata hivyo, alisema wagombea waliojitokeza lazima wafahamu katika uchaguzi kuna kushinda na kushindwa, hivyo ni muhimu wawe tayari kupokea matokeo na kuyaheshimu badala ya kutoa kauli zinazoweza kuhatarisha amani na utulivu.

"Mimi niko tayari kupokea matokeo yoyote yale na niko tayari kufanya kazi na kumpa ushirikiano mgombea yeyote atayetangazwa kuwa Rais wa Zanzibar," alisema Khatib ambaye ni Waziri asiye na Wizara Maalum Zanzibar.

Naye Jecha alisema matayarisho ya uchaguzi wa mwaka huu yamekwenda vizuri na kuwapongea viongozi na watendaji wa tume kwa kufanikisha uchaguzi huo. Alisema uchaguzi umefanyika bila ya kujitokeza malalamiko yoyote katika vituo vya kupigia kura huku usalama ukiwa umeimarishwa katika vituo mbalimbali.

"Siwezi kutofautisha uchaguzi huu na uliopita ambao mwenyekiti wake nilikuwa mimi. Lakini kwa mwaka huu matayarisho yalikuwa mazuri na wananchi wengi wamejitokeza kupiga kura," alisema Jecha.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi alisema upigaji kura ulioanza mapema asubuhi, umempa faraja kutokana na utulivu uliotanda vituoni ambao umewezesha wananchi kutumia haki yao ya kupiga kura na kurejea nyumbani kuendelea na shughuli zao.

Alisema serikali kupitia vyombo vyake vya dola itaendelea kulinda usalama wa wananchi na pale itakapobaini ishara au dalili za uvunjifu wa amani haitasita kuwashughulikia mara moja wale wote watakaohusika na vurugu zozote bila ya kujali cheo cha mtu au kiongozi.

Balozi Iddi aliendelea kuwatahadharisha wanasiasa kujiepusha na kitendo cha kujitangazia ushindi na kusisitiza kuwa jukumu hilo linasimamiwa na mamalaka zilizopewa dhamana kwa mujibu wa sheria.



Baadhi ya wananchi wakiwa wamepanga foleni wakisubiri kupiga kura katika kituo cha Garagara, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Huduma mbalimbali zasimama Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HUDUMA muhimu jana zilisimama katika Mji wa Zanzibar zikiwamo usafiri wa daladala, kufungwa kwa maduka na migahawa ya mamalishe kutokana na uchaguzi mkuu na ule wa Zanzibar.

Katika Soko la Darajani, meza nyingi zilionekana bidhaa zikiwa zimefungwa huku maduka machache ya nyama yakionekana kutoa huduma. Pia katika mitaa ya Darajani, Mlandege, Michezani, Kariakoo, hali ilionekana kuwa ya utulivu huku watu wachache wakionekana kutembea barabarani jambo ambalo si la kawaida kabla ya uchaguzi.

Upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya intaneti na huduma za fedha kupitia simu za mkononi zilikuwa shida kupatikana kutokana na mawakala wengi kufunga maduka yao.

"Leo usafiri umekuwa wa shida, nipo muda mrefu hapa kituoni, lakini magari ya Mpendae siyaoni, alisema Mtumwa Haji.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, kutokana na hali hiyo, aliwataka wafanya biashara kuondoa hofu na kurejesha huduma baada ya kupiga kura ili wananchi wapate mahitaji.

Alisema hali ya usalama inaendelea vizuri na wananchi wamejitokeza kupiga kura bila kupata usumbufu wa aina yoyote.

Nao askari polisi na wale wa vyombo vingine vya usalama, walionekana kufanya doria wakiwa katika magari na pikipiki na kupita katika mitaa mbalimbali ya Mji wa Zanzibar na vitongoji vyake.

Kwa upande wa usafiri wa baharini, huduma zilisitishwa kwa siku moja ili kutoa nafasi kwa wananchi kwenda kupiga kura.

# Wenye ulemavu wasifu mazingira uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA za Watu wenye Ulemavu Zanzibar, zimesema mazingira ya upigaji kura yalikuwa mazuri hasa katika suala la amani pamoja na vifaa vya upigaji kura kwa watu wenye mahitaji maalum licha ya kujitokeza kwa baadhi ya kasoro.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Jumuiya ya Watu Wasioona Zanzibar, Adil Muhammed Ali, alisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (ZEC) na ile ya Zanzibar (ZEC) zimejitahidi kuweka mazingira mazuri ambayo yamewawezesha watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kushiriki uchaguzi bila matatizo.

Hata hivyo, alisema karatasi za kura za wabunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hazikuwa na maandishi ya alama za nukta nundu na badala yake zimewekwa namba, jambo ambalo limesababisha kusomewa na mtu.

"Karatasi za wapigakura wa wagombea wa urais, uwakilishi na madiwani zilikuwa na mfumo mzuri ambao umeturahisishia sisi tusioona kupiga kura wenyewe bila msaada tofauti na karatasi za kura za ubunge," alisema.

Omar Ali, mlemavu wa viungo, alisema utaratibu wa kuingia katika vituo ulikuwa mzuri kutokana na kupewa kipaumbele maalum watu wenye ulemavu.

Pia alisema mazingira ya amani na utulivu yamewapa moyo zaidi kwa kujitokeza kupiga kura tofauti na hali ilivyokuwa katika uchaguzi wa kura ya mapema.

"Jana (juzi) hali haikuwa shwari. Sisi watu wenye ulemavu tulikua na hofu kubwa kwa siku ya leo (jana), lakini hali ni tofauti mazingira yanaruhusu kutoka nyumbani na kwenda kituoni kupiga kura," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Saadat, alisema amepokea malalamiko kutoka kwa watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) viziwi kwamba kutokana na ulemavu wao kutoonekana, walishindwa kuaminika na wengine kurejeshwa na polisi licha ya kuwa na vitambulisho maalum vya ZEC.

"Tume ya Uchaguzi imetoa vitambulisho maalum kwa watu wenye ulemavu, ili wanapoenda vituoni kupiga kura wasipate usumbufu, lakini baadhi ya askari polisi walioko vituoni walishindwa kuwaamini kwa sababu ulemavu si wa kuonekana na wengine kurejeshwa," alisema.

Hata hivyo, alisema amechukua juhudi za kuwasiliana na tume za uchaguzi kuhusu malalamiko hayo, ili kuhakikisha watu wote wenye ulemavu wa uziwi wanaondolewa vikwazo na kupata haki yao ya kikatiba na kidemokrasia ya kushiriki uchaguzi.

## HABARI PICHANI

# MATUKIO YA UPIGAJI KURA ZANZIBAR



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADC, Hamad Rashid Mohamed, akipiga kura katika kituo cha Fidel Casro, Jimbo la Wawi, Pemba jana. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**




Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Mussa Haji Kombo, akipiga kura katika kituo cha Wara Kilimo Mchaomanne, Jimbo la Wawi jana.



Baadhi ya wananchi wa Jimbo la Wawi, Wilaya ya Chakechake, wakipiga kura katika kituo cha Wawi B.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Wakulima Tanzania (AFP), Said Soud Said, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kupiga kura katika kituo cha Wawi, jana.



Baadhi ya kinamama wa Jimbo la Kojani, Wilaya ya Wete, wakiwa katika foleni kusubiri kupiga kura katika kituo cha Kangagani, Jimbo la Kojani, jana.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha NRA, Khamis Faki Mgau, akipiga kura katika kituo cha Kangagani, Jimbo la Kojani jana.

HABARI KIMATAIFA

# Wamarekani milioni 70 wapiga kura kwa posta

**WASHINGTON, Marekani**

ZAIDI ya Wamarekani milioni 70 tayari wamepiga kura kwa njia ya posta katika uchaguzi wa urais wa Novemba 3, sawa na zaidi ya nusu ya jumla ya waliojitokeza katika uchaguzi wa mwaka 2016.

Hii ni wiki moja kabla ya siku ya uchaguzi, kulingana na takwimu zilizotolewa na U.S. Elections Project.

Idadi hiyo, ambayo inaonyesha kasi ya rekodi ambayo inaweza kusababisha idadi kubwa zaidi ya wapiga kura katika zaidi ya karne moja, ni ishara ya hivi karibuni ya nia kubwa katika vita kati ya Rais wa kutoka chama cha Republican, Donald Trump na mpinzani wake wa kutoka chama cha Democratic, Joe Biden.

Pia idadi hiyo inaonyesha hamu ya wapiga kura kupunguza hatari ya kuambukizwa virusi vya Corona wakati kunaripotiwa mlipuko mpya wa janga hilo, huku msimu wa baridi ukikaribia.

Kwa ujumla, chama cha Demokratic kina nafasi karibu mbili kwa moja katika idadi ya kura za mapema.

Hata hivyo chama cha Republican kimepunguza pengo kupitia upigaji kura wa mapema kwa mtu katika wiki za hivi karibuni, kama zinavyoonyesha takwimu zilizokusanywa, kulingana na shirika la habari la Reuters.

***RFI***



Moja ya duka mjini Philadelphia nchini Marekani, ambalo limevamiwa na wezi baada ya ghasia kuzuka polisi walipompiga risasi na kumuua mtu mweusi.**PICHA: REUTERS**

## Mkataba wa kusitisha vita Libya wasainiwa

**NEW YORK, Marekani**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa limeidhinisha mkataba wa kusitisha vita uliosainiwa kati ya pande zinazohasimiana nchini Libya mwishoni mwa wiki iliyopita.

Wanadiplomasia wameipongeza hatua hiyo na baraza hilo limezitaka pande zote kuyatekeleza makubaliano hayo kikamilifu.

Duru ya kidiplomasia imeeleza kuwa kuidhinishwa kwa makubaliano hayo kutafuatiliwa na azimio la Umoja wa Mataifa.

Baraza hilo pia limezitaka pande mbili husika, kujitolea kupata suluhisho la kisiasa watakapokutana kujadili masuala zaidi Novemba 9, nchini Tunisia.

Pande zinazozozana Libya zilisaini mkataba wa kusitisha vita baada ya mazungumzo yaliyodumu kwa siku tano mjini Geneva nchini Uswizi chini ya Umoja wa Mataifa.

***DW***

# Ujerumani kufunga baa kukabiliana na corona

**BERLIN, Ujerumani**

UJERUMANI inatarajia kuweka masharti mapya ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona kwa kufunga baa na maeneo mengine ya kuuza vileo.

Hatua nyingine ambayo imepanga kuchukua ni kupunguza mikusanyiko ya kijamii kwa kiasi kikubwa.

Mipango hiyo iliwasilishwa jana wakati Kansela Angela Merkel akizungumza na mawaziri wakuu wa majimbo 16 nchini humo katika mkutano wa video.

Chini ya kanuni hizo mpya, ambazo huenda zikaanza kutekelezwa Novemba 4 hadi mwisho wa mwezi huo, watu wataruhusiwa kukutana katika maeneo ya umma na jamaa zao wanaoishi katika nyumba moja na kaya nyingine moja.

Baa, vilabu na maeneo ya aina hiyo yatafunguliwa kwa ajili ya huduma za kununua bidhaa za kufungiwa.

Shule na vituo vya malezi ya watoto vitaendelea kutoa huduma lakini chini ya kanuni mpya za usafi.

Tangu kuanza kwa janga hilo, watu wapatao 450,000 wameambukizwa nchini Ujerumani na waliokufa ni zaidi ya 10,000.

***DW***

# Iran yajenga mtambo wa nyuklia

**TEHRAN, Iran**

PICHA za satelaiti ambazo zimetolewa jana zimeonyesha nchi ya Iran imeanza ujenzi katika eneo lake la mtambo wa nyuklia la Natanz.

Ujenzi huo unakuja wakati Marekani inakaribia kufanya uchaguzi mkuu.

Shinikizo kutoka kwa Rais Donald Trump limeifanya Iran kuachana na masharti kuhusu mpango wake wa zana za nyuklia.

Wachunguzi wa masuala ya atomiki wa Umoja wa Mataifa wamethibitisha kuwa nchi hiyo imeanza kujenga mtambo wa kisasa chini ya ardhi, baada ya mtambo wake wa awali kulipuka, katika kile Iran ilidai lilikuwa shambulizi la hujuma.

Mkuu wa shirika hilo la atomiki, Rafael Grossi ameliambia Associated Press kuwa Iran pia inaendelea kuhifadhi madini mengi ya urani yenye rotuba ya chini, lakini haionekani kumiliki za kutosha kwa ajili ya kutengeneza silaha.

**DW**

# Obama amvaa Trump usimamizi wa corona

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa zamani nchini Marekani, Barack Obama, anaendelea na kampeni kwa niaba ya Makamu wake wa zamani Joe Biden huku akilaumu usimamizi wa Donald Trump dhidi ya corona.

Katika kampeni yake huko Orlando, Florida juzi, Obama alitoa lawama hizo dhidi ya Rais Trump, ikiwa ni wiki moja nchi hiyo kupiga kura za uchaguzi mkuu.

Akizungumza huko Orlando mbele ya magari ya wafuasi wake, badala ya kumshangilia kwa kupiga makofi, walipiga honi wakati wote alipomshambulia Trump kwa namna anavyoshughulikia janga hilo.

“Siku nyingine kwenye mkutano alisema kwamba watu wanatilia maanani corona. Huenda alikuwa na wivu kuona namna taarifa mbalimbali kuhusu ugonjwa huu hatari zikirushwa kwenye vyombo vya habari, kauli aliyotumia siyo sahihi kwa kiongozi kama yeye,” alisema Obama Shutuma kama hizo hazijawahi kutokea katika nchi ambayo ni kawaida kwa Rais wa zamani kutomkosoa mrithi wake.

Lakini, baada ya kukaa kimya kwa mashambulizi ya Trump kwa karibu miaka minne, Obama ameamua kuvunja utamaduni huo katika siku za mwisho za kampeni.

Kampeni hiyo ilirushwa moja kwa moja na vituo vyote vya habari, hata kituo cha Fox News kilicho karibu na Rais Trump kiliirusha.

Hii ni kampeni ya tatu ya Obama kwa kuunga mkono makamu wake wa zamani.

“Lengo siyo kukusanya wapiga kura wapya bali kuhamasisha wapiga kura wa chama cha Democratic. “Lazima mwende kupiga kura, msiwe wavivu kama mwaka 2016 ili tuweze kumuangusha Trump,” alisema Obama.

**Rfi**

# ZIDANE

## TUTAKUWA MAKINI NA HAZARD




**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema 'Los Blancos' hao watakuwa makini mno na Eden Hazard baada ya kurudi kutoka chumba cha majeruhi na kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hazard alitoka benchi na kuingia uwanjani zikiwa zimebakia dakika 20 wakati mabingwa hao wa LaLiga walipolazimishwa sare ya mabao 2-2 na Borussia Monchengladbach, shukrani kwa Casemiro aliyesawazisha dakika ya 93.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alijumuishwa kwenye kikosi hicho kwa mara ya kwanza msimu huu, baada ya kuumia misuli.

Akizungumzia kurudi kwa Hazard dimbani, Zidane aliwaambia waandishi wa habari: "Ulikuwa mchezo wake wa kwanza baada ya muda mrefu.

"Huo ulikuwa mpango wetu kujaribu kumrudisha uwanjani na kumpa nafasi ya kucheza na ndicho tulichokifanya.

"Anahitaji kupewa nafasi ya kucheza mara kwa mara na hiyo itategemea na mchezo uliopo mbele yetu.

"Lakini tutakuwa makini zaidi katika kumpa nafasi ya kucheza, kwa sababu hatutaki tena kuwa kwenye hatari ya kumfanya aumie tena."

# GUARDIOLA

## AAHIDI MAN CITY KUBADILIKA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amebainisha kwamba, Manchester City lazima ikubali shutuma baada ya kuwa na mwanzo mbaya kwenye Ligi Kuu ya England, lakini hana shaka kikosi chake kitarudi kwenye ubora wake.

Baada ya kutoka sare ya 1-1 na West Ham Jumamosi, City imepata pointi nane tu katika mechi zake tano za ufunguzi za Ligi Kuu msimu huu, wakiwa na mwanzo mbaya zaidi tangu msimu wa 2014-15.

City, ambao watacheza na Sheffield United Jumamosi, imepitwa pointi tano na vinara Everton na Liverpool, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Hata hivyo, mambo yamekuwa tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ferran Torres, Ilkay Gundogan na Raheem Sterling, kila mmoja alifunga bao wakati Man City wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Marseille, Jumanne.

Wakati Guardiola akikubali shutuma dhidi yake, anaamini timu hiyo inaonyesha ishara chanya kwamba itarudi kwenye kiwango chake ndani ya miezi michache inayokuja.

"Hapana," alijibu Guardiola wakati alipoulizwa na BT Sport kama shutuma dhidi ya City zimekuwa zikimuumiza.



"Tunatakiwa kuikubali hali hii. Leo hii soka la dunia lipo kwenye mitandao ya kijamii, na tunacheza kila baada ya wiki tatu, hivyo shutuma lazima ziwe nyingi kutokana na kiwango cha timu.

"Hivyo tunatakiwa kukubali shutuma hizi, lakini naamini timu itarudi kwenye kiwango chake ndani ya muda mfupi."

# SIMEONE AKUNWA KIWANGO CHA JOAO



**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone amesifia kiwango cha Joao Felix baada ya mabao yake mawili kuisaidia Atletico Madrid kuibuka na ushindi wa 3-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Salzburg, Jumanne.

Kikosi hicho cha Simeone kilirudi kwa staili yake katika mashindano hayo baada ya wiki iliyopita kucheza kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Bayern Munich kwenye mchezo wa kwanza wa Kundi A wa michuano hiyo.

Joao mwenye umri wa miaka 20, alifunga bao lake la kwanza na kufanya matokeo kuwa 2-2, kabla ya kufunga la pili na kuihakikisha Atletico pointi zote tatu.

Simeone alifurahishwa zaidi na kiwango cha nyota huyo wa kimataifa wa Ureno na kusema alikuwa kwenye ubora wake.

"Kama ataendelea kuonyesha majukumu yake, kasi na kufanya maamuzi kama alivyofanya leo ataendelea kukua vizuri sana," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tuna matumaini tunaweza kumsaidia yeye kwa sababu naamini Joao Felix atakuwa bora zaidi kwa siku zijazo.

"Kiwango chake ndicho kilichoamua matokeo kwenye mchezo wetu na nina imani kubwa naye."



# CONTE

## HANA SHAKA KIWANGO CHA INTER

# KIMMICH: BAYERN INABAHATI KUSHINDA

**MOSCOW, Urusi**



JOSHUA Kimmich amesema mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Bayern Munich walikuwa na "bahati" kupata ushindi ugenini baada ya kufunga bao wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Lokomotiv Moscow.

Kimmich alifunga bao hilo dakika ya 79 na kuwafanya Bayern kushinda mechi ya 13 mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lokomotiv ilianza kuwa nyuma kwa bao la Leon Goretzka alilofunga dakika ya 13, kabla ya Anton Miranchuk kusawazisha kwenye mchezo huo uliopigwa Jumanne.

Kimmich alifunga bao hilo la ushindi katika mchezo huo ambao Lokomotiv walionekana kuwa kwenye ubora zaidi.

"Nafikiri Lokomotiv walikuwa kwenye kiwango bora zaidi," alisema Kimmich baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Walikuwa kwenye ubora mzuri zaidi, safu yao ya mashambulizi ilikuwa nzuri na tulikuwa kwenye wakati mgumu.

"Kipindi cha pili kilikuwa kigumu sana kwetu na kwa uhakika tulikuwa na bahati kuibuka na ushindi kwenye mchezo huu."

**DONETSK, Ukraine**

ANTONIO Conte amesema aliridhika na kiwango cha Inter Milan wakati wakitoka sare ya bila kufungana na Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Inter iliifumua Shakhtar mabao 5-0 kwenye Ligi ya Europa hatua ya nusu fainali Agosti, lakini vijana hao wa Conte wakashindwa kufurukuta pale kwenye dimba la Kiev Olympic.

Inter imebakiwa bila ushindi kwenye kundi lake la B baada ya wiki iliyopita kutoka sare ya 2-2 na Borussia Monchengladbach na sasa itakabiliana na mabingwa wa LaLiga, Real Madrid kwenye mchezo ujao.

Conte baada ya mchezo huo alisema Inter ipo kwenye mstari sahihi na kwamba ana imani kubwa kikosi hicho kitakuwa bora.

"Naona ishara nzuri kwa kikosi kwa sababu timu inacheza vizuri na tupo katika njia sahihi kabisa," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tulikuwa na mchezo mgumu na wapinzani wetu walikuwa kwenye kiwango bora kabisa.

"Nina imani timu ipo kwenye njia sahihi kabisa na nina waamini wachezaji wangu na mechi zijazo tutapata ushindi."



# BARTOMEU AJIUZULU URAIS BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amejiuzulu nafasi hiyo, klabu ya nchini Hispania imethibitisha.

Miamba hao wa LaLiga walitangaza Jumanne kwamba, Bartomeu na bodi yote ya wakurugenzi wamejiuzulu baada ya kumalizika kwa mkutano wao.

Jumatatu wiki hii, Bartomeu alisisitiza kwamba hana sababu ya kujiuzulu kuelekea kupigiwa kura ya kutokuwa na imani na uongozi wake, ambapo ilitarajiwa kupigwa mwishoni mwa wiki hii pale Camp Nou.

Hata hivyo, Bartomeu mwenye umri wa miaka 57, alibadilisha uamuzi wake na kuamua kujiuzulu katika nafasi yake hiyo.

Katika taarifa ya Jumanne, Bartomeu alitangaza: "Nimeamua kujiuzulu katika nafasi ya urais mimi na bodi yangu yote."

Taarifa hiyo imekuja na kuwa ndio mwisho wa presha kubwa iliyokuwapo ndani ya klabu hiyo kwa muda mrefu.

Bartomeu ambaye awali alikuwa makamu wa rais, alichaguliwa kuwa rais wa klabu hiyo mwaka 2014 baada ya Sandro Rosell kujiuzulu kwa madai ya kusababisha Neymar kuondoka klabuni hapo.

Barca ilifurahia mafanikio katika mwaka wa kwanza wa Bartomeu, ikishinda mataji matatu chini ya kocha, Luis Enrique msimu wa 2014-15 na ndio mara ya mwisho kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Bartomeu alishinda kwa asilimia 54.63 ya kura zote.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED KUIFUATA LIVER SAINI YA UPAMECANO

Bayern Munich, Real Madrid nazo mbio moja kwa nyota huyo wa RB Leipzing ambaye mkataba wake...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imepanga kwenda kutoa upinzani kwa Liverpool, Bayern Munich na Real Madrid katika mbio za kuipata saini ya nyota wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, na itaanza kwa kushawishi kupunguziwa bei ili iweze kumsajilii, kwa mujibu wa gazeti la The Times.

Upamecano amekuwa mchezaji anayewaniwa na klabu nyingi barani Ulaya baada ya kujiimarisha yeye mwenyewe pale RB Leipzig.

Upamecano awali alionekana kwamba angeondoka kwenye klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Julai mwaka huu kabla ya kuongeza mkataba.

Man United awali ilihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo, kabla ya dili hilo kushindikana.

United inapanga kuimarisha safu yake ya ulinzi na 'Mashetani Wekundu' hao wanamuona Upamecano kuwa ndio mtu sahihi kwao.

Hata hivyo, klabu za Liverpool, Bayern Munich, Real Madrid na Barcelona nazo zimekuwa zikimtolea macho nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Upamecano alisaini mkataba mpya Julai mwaka huu, na mkataba wake una kipengele cha kuondoka kwa pauni milioni 38.

## KWA UFUPI

**LIVERPOOL KWA JOHANNESSON**

LIVERPOOL inamfuatilia kiungo wa Iceland, Isak Bergmann Johannesson mwenye umri wa miaka 17, ambaye anaichezea IFK Norrkoping ya nchini Sweden. ***(Expressen)***

**FATI ATAJWA JUVENTUS**

JUVENTUS ilijaribu kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 17, katika dirisha la usajili la majira ya joto lililopita. ***(Calcio Mercato)***

**BRIGHTON YAIZUIA BAYERN**

KLABU ya Brighton imempa mkataba mpya mlinzi wake, Tariq Lamptey, mwenye umri wa miaka 20, wakati huu akihusishwa na Bayern Munich. ***(Sun)***

**MBAPPE KWENDA MADRID**

NYOTA wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, atatimkia Real Madrid katika dirisha lijalo la usajili la majira ya joto, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani wa timu ya Taifa ya Vijana ya Ufaransa chini ya miaka 21, Adil Rami. ***(Metro)***

**LUCIEN AMFUNGUKIA SANCHO**

KOCHA wa Borussia Dortmund, Lucien Favre, anaamini kwamba uvumi kumhusu winga, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20 kuelekea Manchester United, ungeweza kusababisha kushuka kwa kiwango kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa England. ***(Mirror)***

**MARTINEZ HAJUI HATIMA YAKE**

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lautaro Martinez, mwenye umri wa miaka 23, hajui nini kitatokea kuhusu mustakabali wake, lakini kwa sasa amesema ana furaha kucheza pale Inter Milan. ***(AS)***

**MAHREZ KURUDI MARSEILLE**

WINGA wa Manchester City raia wa Algeria, Riyad Mahrez, mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari siku moja kurejea Ufaransa kuchezea klabu yake ya utotoni ya Marseille. ***(Sun)***

**BARCELONA KUMSAJILI MALEN**

BARCELONA itajaribu kumsajili mshambuliaji wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Donyell Malen, mwenye umri wa miaka 21, kama itashindwa kukamilisha usajili wa Memphis Depay. ***(Mundo Deportivo)***

**ROMERO AITWA RACING**

GOLIKIPA wa Manchester United, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, amepewa ofa ya kurejea Racing Club de Avellaneda, lakini itampasa akubalia kukatwa mshahara wake kwa kiwango kikubwa. ***(Star)***

**EDU KAMPIKU ARTETA ARSENAL**

MKURUGENZI wa ufundi wa Arsenal, Edu, alimpiku kocha Mikel Arteta katika kumsajili, Thomas Partey, mwenye umri wa miaka 27, badala ya kiungo Mfaransa mwenye miaka 22 kutoka Lyon, Houssem Aouar. ***(L'Equipe)***

**BODI YA LIGI EPL INA JAMBO**

BODI ya Ligi Kuu England itajiweka kando katika juhudi zake za kuishawishi Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi hiyo kuleta visa maalumu, baada ya Engalnd kujiondoa rasmi Umoja wa Ulaya. ***(Mail)***

**WEST BROM YAMKERA BILIC**

KOCHA wa West Brom, Slaven Bilic, amekasirishwa na mtendaji mkuu wa klabu hiyo baada ya kumruhusu mlinzi wa Misri, Ahmed Hegazi mwenye umri wa miaka 29, kuondoka na kujiunga na Al-Ittihad inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudi Arabia, bila yeye kujua. ***(Sun)***

# ADAM AFICHUA SIRI YA 'HAT-TRICK' YAKE

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI wa kwanza wa mabao matatu kwenye mechi moja ('hat-trick') msimu huu, Adam Adam, amesema kabla ya mchezo huo alikuwa akiwaeleza wachezaji wenzake atafunga idadi hiyo ya magoli.

Akizungumza na gazeti hili jana, Adam, straika wa JKT Tanzania, alisema amepokea kwa furaha si tu kufunga 'hat-trick', lakini pia kuwa mchezaji wa kwanza msimu huu wa 2020/21 kufanya hivyo, pamoja na kuisaidia timu yake kupata ushindi.

Jumapili iliyopita, mchezaji huyo alifunga hat-trick katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara akiisaidia JKT Tanzania kushinda mabao 6-1 dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, mjini Shinyanga.

"Nimepokea kwa furaha sana kwa sababu siku moja kabla ya mechi kambini nilikaa na wenzangu nikawa nawaambia kuwa kesho (juzi), nitafunga 'hat-trick'. Nilikuwa nawatania, lakini moyoni mwangu nikawa najiambia mwenyewe naomba iwe kweli na hata nilipoingia nikawa nahaha uwanjani, nilipofunga bao la kwanza nikaona sawa, nilipofunga la pili nikaona kumbe inawezekana, nikawa sasa nahangaika kulipata bao la tatu kwa nguvu zote na kweli nikafunga," alisema Adam.

Alisema alipofunga bao lake la tatu kwenye mechi hiyo, wachezaji wenzake walimfuata na kumpongeza wakimuuliza maswali kuwa jana aliwaambia hivyo, je, alijuaje kama angefunga?

Alisema kutokana na kufunga idadi hiyo ya mabao na kufikisha magoli manne kwa msimu huu, sasa ameingia rasmi kwenye kinyang'anyiro cha kuwania Kiatu cha Dhahabu.

"Mwanzo tulikuwa na upepo mbaya, lakini ukiangalia wachezaji wote wa JKT Tanzania ni wale wale wa msimu uliopita ambao tulifanya vizuri, lakini kwa sasa tumerudi vizuri," alisema straika huyo.

Adam alifunga hat-trick hiyo dakika ya 23, 48, na 83, huku mabao mengine mawili yakifungwa na Daniel Lyanga dakika ya 44 na 52 na goli la sita likipachikwa wavuni na Said Luyaya kwenye dakika tatu za nyongeza kabla ya mechi hiyo kumalizika.

Bao pekee la kufutia machozi la Mwadui lilifungwa na Pastor Athanas dakika ya 62.

Mchezaji wa kwanza kufunga 'hat-trick' msimu uliopita alikuwa ni Ditram Nchimbi wakati huo akiichezea Polisi Tanzania katika mechi dhidi ya Yanga, klabu ambayo kwa sasa anaitumikia ambapo mchezo huo ulimalizika kwa sare ya mabao 3-3.

**YALAAAH...**




Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, akiugulia maumivu baada ya kuchezewa ndivyo sivyo wakati akikokota mpira kuelekea langoni mwa Midtjylland kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi iliyopigwa Uwanja wa Anfield usiku wa kuamkia jana na Liverpool kushinda 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Mbeya City yaanza kuchonga Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Mbeya City imesema matokeo hayo yanatokana na 'mageuzi' na mabadiliko kadhaa ambayo yamefanywa na viongozi kwa manufaa ya klabu hiyo.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Emmanuel Kimbe alisema timu yao imeanza kufanya vizuri baada ya wao kama viongozi kufanya uamuzi mgumu na wanafurahi kuona 'matunda' yake yameanza kuonekana.

Kimbe alisema bado timu yao itaendelea kuwa chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Mathias Wandiba, mpaka pale mwalimu mpya atakapopatikana.

"Wandiba ataendelea kufundisha hadi hapo kocha mkuu atakapopatikana, tumepokea maombi mengi kutoka sehemu mbalimbali, lakini muda wa kufanya uamuzi haujafikiwa, bado tupo katika mchakato, ukikamilika tutawatangazia, kwa sasa hatuwezi kusema kama anatoka nje au wa hapa hapa ndani," Kimbe alisema.

Jumapili iliyopita, ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Mbeya City ilipata ushindi wake wa kwanza msimu huu illipoichapa Kagera Sugar mabao 2-1.

Tangu kuondoka kwa aliyekuwa Kocha Mkuu, Amri Said, Mbeya City ilianza kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Dodoma Jiji, ikapoteza kwa kufungwa kwa 'mbinde' mabao 2-1 na Mwadui, kabla ya kupata ushindi wa kwanza wa 2-1.

Kabla ya hapo, Mbeya City ilianza kwa kupoteza mechi nne mfululizo kisha kupata sare ya kwanza dhidi ya Prisons pamoja na Dodoma Jiji, na ilipochapwa mabao 2-1 dhidi ya Mwadui, uongozi wa Mbeya City uliamua kumuachisha kazi kocha Amri na nafasi yake kuchukuliwa na kocha huyo msaidizi.

Mpaka sasa Mbeya City inashika nafasi ya 17, ikiwa na pointi tano, baada ya kushuka dimbani mara nane.

## Dante nje KMC ikiivaa Gwambina

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kukubali kichapo kutoka kwa Yanga, uongozi wa KMC FC umesema kikosi chake kimesharekebisha makosa yake na sasa wanawaza 'kuvuna' pointi tatu watakapokutana na Gwambina FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa KMC FC, Christina Mwagala, alisema wamefanya mazoezi na kushiriki programu tofauti ambazo zimelenga kuwaimarisha kuelekea mechi hiyo.

Mwagala alimtaja mchezaji ambaye ni majeruhi na atakosekana katika mechi hiyo kuwa ni beki Andrew Vincent 'Dante', ambaye aliumia kwenye mchezo uliopita dhidi ya Yanga.

"Tumeshafunga ukurasa wa mechi iliyopita, sasa tunaendelea na maandalizi kuhakikisha tunapata matokeo mazuri ambayo ni kuondoka na alama tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu," Mwagala alisema.

Aliongeza kuwa bado uongozi wa timu hiyo unaliamini benchi la ufundi na wachezaji wote katika vita waliyokuwa nayo ya kuwania ubingwa msimu huu.

KMC FC ina pointi 11 baada ya kushinda mechi tatu, sare mara mbili na imepoteza michezo mitatu.

## Gwambina yatamba mastraika 'wameiva'

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, amesema mabadiliko aliyoyafanya kwenye safu yake ya ushambuliaji yanampa 'jeuri' ya kujiamini kuibuka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Misungwi jijini Mwanza.

Fulgence aliliambia gazeti hili jana maandalizi ya kikosi chake yamekamilia na yanampa imani ya kupata alama tatu muhimu katika mechi hiyo ambayo wao ni wenyeji.

Kocha huyo alisema wachezaji wana ari kubwa na kila mmoja anataka kuona wanatumia vema uwanja wa nyumbani na kuendelea kukaa kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi.

Alisema shida kubwa ilikuwa washambuliaji wake kumalizia nafasi wanazotengeneza, jambo ambalo amelifanyia kazi na sasa kikosi chake kipo vizuri na kuhakikisha wanapata pointi muhimu katika mchezo huo.

"Kikosi changu kipo fiti, ninafurahi safu ya umaliziaji imeimarika, kulingana na nilivyoiona KMC nina imani wanafungika, kwa sababu ukiangalia timu walizotoka nazo sare katika mechi zilizopita ikiwamo Polisi Tanzania na Kagera Sugar, sisi tumezifunga timu hizo," alisema Fulgence.

Aliongeza kuwa katika Ligi Kuu Bara hakuna mechi rahisi, lakini anafurahi kuona wachezaji wake wanaendelea kuimarika kutokana na aina ya mazoezi anayowapa.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 29, 2020

Nipashe




UNITED KUIFUATA LIVER SAINI YA UPAMECANO

HABARI UK 22

WAMEREJEA...



Washambuliaji wa Simba, Chris Mugalu na Meddie Kagere (katikati) ambao wameanza mazoezi baada ya kupona majeraha waliokuwa wakiuguza, wakiwa na kiungo wa timu hiyo Clatous Chama (kulia), ambaye naye alikosekana katika mechi mbili ambazo timu yao ilipoteza dhidi ya Tanzania Prisons na Ruvu Shooting. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA: MAJEMBE SASA YAMEREJEA

●●●Ni nyota watano wa kikosi cha kwanza, Mkenya aongezwa benchi la ufundi huku Abbas akipewa...

**Na Somoe Ng'itu**

WACHEZAJI nyota wa mabingwa watetezi, Simba wanatarajia kurejea katika kikosi cha kwanza kitakachoivaa Mwadui FC kutoka Shinyanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Simba imepoteza mechi mbili mfululizo kwa kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa 'Maafande' wa Tanzania Prisons na baadaye dhidi ya Ruvu Shooting, na kuwafanya mabingwa hao kupoteza jumla ya pointi sita.

Nyota ambao walikosekana katika mechi dhidi ya Tanzania Prisons na Ruvu Shooting, ni pamoja na Clatous Chama, Meddie Kagere, Paschal Wawa, Chriss Mugalu na John Bocco ambaye alianzia benchi kwenye mchezo uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmoja wa viongozi katika benchi la ufundi, alisema kukosekana kikamilifu kwa wachezaji hao kulikiathiri kikosi chao, lakini anaamini hali hiyo haitajirudia kwenye mechi inayofuata hapo Jumamosi.

Kiongozi huyo alisema wachezaji wote wamefanya mazoezi vizuri kuanzia juzi na leo wanatarajia kuendelea kujiimarisha kuhakikisha wanapata matokeo ya ushindi na kuwaondolea 'machungu' mashabiki na wanachama wa Simba.

**"Kupoteza wachezaji watano wa kikosi cha kwanza halikuwa jambo dogo, huwezi kupata ushindi kama huna mastraika, na kwa mchezo wa Sumbawanga hatukustahili matokeo yale, kama refa angekuwa 'fair' labda tungeshinda au hata tungeambulia sare.**

"Kuhusu mechi ya juzi (Alhamisi) na Ruvu, hii tulicheza katika kiwango cha chini, lakini tatizo liko pale pale, huwezi kupata matokeo mazuri kama huna robo tatu ya wachezaji wako wa kikosi cha kwanza, kukosa watu wa mbele kulituathiri kwa kiwango kikubwa," alisema.

Aliendelea kueleza kuwa wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na hofu kuelekea mechi zinazofuata kwa sababu matokeo mazuri yatarejea baada ya hali za 'majembe' yao yaliyokuwa majeruhi kuimarika.

**ABBAS MENEJA MPYA**

Taarifa za ndani za klabu hiyo zinasema aliyekuwa Mratibu, Abbas Ally, anatarajiwa kukaimu nafasi ya Patrick Rweyemamu, ambaye alitimuliwa kwenye nafasi ya umeneja wa timu hiyo.

Chanzo hicho pia kiliendelea kusema kocha wa zamani wa makipa, Mkenya Iddi Salim, naye anatarajiwa kutua klabuni hapo kuchukua mikoba ya Mohammed Mwarami, ambaye amekalia 'kuti kavu'.

"Kwa leo (jana), hakuna mpya, tumepewa ruhusa ya kwenda kupiga kura na jioni tutarejea kambini kuendelea na maandalizi ya mchezo wetu wa Jumamosi, tumeumia na tunaahidi tutawafuta machozi katika mechi ya Mwadui, tunajua upepo umechafuka," chanzo chetu kiliongeza.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba yenye pointi 13, iko nafasi ya nne nyuma ya vinara Azam FC yenye pointi 21, Yanga yenye pointi 19 na Biashara United yenye pointi 16.

Baada ya mechi ya keshokutwa, Simba itaendelea kubakia Dar es Salaam na Novemba 4, mwaka huu itawakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa katika Uwanja wa Uhuru jijini.

## BIASHARA YAJITOA HOFU KWA YANGA

**Na Saada Akida**

LICHA ya wachezaji wake wanne tegemeo kuwa katika hatihati ya kushuka dimbani Jumamosi kuikabili Yanga, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, amesema hawahofii na hawaogopi vigogo hao ambao watawakaribisha kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara hapo keshokutwa.

Baraza alisema ana asilimia kubwa ya kuwakosa baadhi ya wachezaji wake nyota, akiwamo straika tegemeo Daniel Mgore, Abdul Mangalo, Ally Kombo na Gerald Mdamu.

Kocha huyo alisema kwa sasa wachezaji hao wapo katika uangalizi mkubwa huku leo akitarajia kupata taarifa kamili kutoka kwa daktari wa timu hiyo.

Alisema ni pigo kwake kuwakosa nyota hao ila haitaathiri mipango yake kuelekea mchezo wao dhidi ya Yanga kwa sababu, tayari ameshawaanda wachezaji wake kiufundi na kisaikolojia kuhakikisha wanapata pointi muhimu katika mechi hiyo.

"Sina uwoga kabisa na Yanga, kulingana na maandalizi ambayo ninaendelea kuyafanya, nina imani itakuwa mechi ya ushindani mkubwa, kutokuwapo kwa nyota wangu muhimu wasifikiria watapata mteremko kwa kupata matokeo rahisi.

"Nimeiona Yanga ikicheza chini ya huyo kocha wao mpya (Cedric Kaze), amebadilisha mfumo wanacheza kwa kuweka mpira chini, kwangu ni rahisi kwa sababu wote tutakuwa tunacheza mpira wa kisasa, kwa mfumo huo umenipa matokea mazuri mechi zetu zilizopita," alisema Baraza.

Alisema kiufundi timu yake ipo vizuri kukabiliana na Yanga, na analiheshimu benchi la ufundi pamoja na wachezaji wa Yanga ila amejipanga kuhakikisha wanazuia pointi muhimu nyumbani kwao.

"Sina presha wala kutishika na safu ya ushambuliaji ya Yanga, haina tofauti na safu yangu ya ushambuliaji sababu ukiangalia mechi nyingi za wapinzani wangu hao idadi yao ya kufunga ni bao moja moja kama ilivyo kwa washambuliaji wangu kufunga idadi hiyo hiyo," alisema Baraza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002